

**MAUAJI ANETH MSUYA**

Mke wa Bilionea Msuya aibua hoja, Jamhuri yaomba muda ikajipange

UKURASA 7



**UTAFITI** wabaini wanaoanza pombe chini ya umri miaka 15 wako hatarini zaidi

UKURASA 15


# Nipashe

Jumamosi Oktoba 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581477

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**ONANA AFUNGUKA GARNACHO HAJAKOSEA**

UKURASA 22




## Idara zenye ajira zinazohitaji waombaji serikalini hizi hapa

UKURASA 9

**HARUFU YA RUSHWA**

# Bati moja lanunuliwa bei 'kufuru' serikalini



**TAKUKURU** yashtukia mchezo mchafu; miamala ya Sh. trilioni 3/- yenye viashiria vya rushwa na udanganyifu yanaswa...

*Endelea Ukurasa wa 3*

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, CP Salum Hamduni

## Majambazi waua mlinzi KKKT, wapora mamilioni

UKURASA 2

**MICHEZO** SHIME AAHIDI MAKUBWA TWIGA IKIENDA BOTSWANA UK. 23 **KATUNI** UK. 6

# Majambazi waua mlinzi KKKT, wapora mamilioni

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MLINZI wa Kampuni ya Ulinzi ya Ironjezi, Shida Matembo, aliyekuwa akilinda eneo la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Msamala, Halmashauri ya Manispaa ya Songea, amefariki dunia katika tukio la ujambazi.

Imeelezwa kuwa mwili wa Matembo (49), mkazi wa Lizaboni Songea, umekutwa ukiwa na majeraha makubwa eneo la tukio huku mlinzi mwingine Severin Mbalale (72), mkazi wa Mletele, Songea naye akijeruhiwa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali mwilini na kundi la watu wanaodhaniwa majambazi.

Inadaiwa kuwa watuhumiwa hao baada ya kumuua Matembo na kumjeruhi mlinzi mwenzake, walivunja maduka mawili kisha kuiba fedha zaidi ya Sh. milioni 15 na pikipiki moja iliyokuwa imeegeshwa nyumbani kwa askofu wa kanisa hilo Dayosisi ya Ruvuma.

Taarifa zilizomfikia mwandishi wa habari hizi na kutolewa ufafanuzi jana mjini hapa na Mkuu wa Jimbo la Ruvuma wa KKKT Dayosisis ya Ruvuma, Mchungaji Mhabuka zinadai kuwa tukio hilo limetokea usiku wa kuamkia juzi katika Kanisa la Usharika wa Msamala.

Mchungaji Mhabuka alidai kuwa watu wanaodhaniwa majambazi, walivamia eneo hilo kisha walivunja vibanda viwili vya wafanyabiashara ambao ni wapangaji ambao majina yao hayajafahamika; mmoja anamiliki duka la uwakala wa taasisi za fedha na mwingine anamiliki duka la vyakula.

Alifafanuwa kuwa kwenye duka la wakala wa taasisi za fedha inadaiwa majambazi hao walifanikiwa kuchukua fedha taslimu zaidi ya Sh. milioni 10 na kwenye duka lingine walipora bidhaa mbalimbali na fedha taslimu zaidi ya Sh. milioni tano.

Alidai kuwa wahalifu hao pia walichukua pikipiki ambayo ilikuwa imeegeshwa nje ya eneo la maegesho ya magari ambalo lipo jirani na nyumbani kwa askofu wa kanisa hilo kisha waliondoka na kutokomea kusikojulikana.

Mchungaji Mhabuka alisema mlinzi aliyeuawa alikuwa analinda maeneo yote ya kanisa pamoja na vibanda vya biashara na mlinzi aliyejeruhiwa alikuwa analinda nyumbani kwa askofu wa dayosisi hiyo.

Alilitaja ni tukio lililosababisha taharuki kubwa kwa kuwa kitendo kilichofanywa ni cha kikatili, hivyo akaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kuwabaini wahalifu hao.

Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma, Dk. Magafu Majura, alithibitisha kupokea mwili wa Matembo.

Alifafanua kuwa mwili huo wamebaini una majeraha mengi. Umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhi maiti. Wanasubiri taratibu za kufanya uchunguzi zaidi.

Dk. Majura pia alithibitisha hopsitali hiyo kumpokea majeruhi Severi Mbalale ambaye amelazwa chumba cha majeruhi, akiendela kupatiwa matibabu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marco Chilya, alipoulizwa na mwandishi wa habari kuhusu tukio hilo, alithibitisha kuwa na taarifa za tukio hilo. Jeshi la Polisi mkoani mwake linaendelea na uchunguzi, likiwasaka wahalifu hao.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akizungumza na Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini Kati – Makete, Dk. Wilson Sanga wakati akikagua chanzo cha maji cha mradi wa kufua nishati ya umeme wa KV 360 unaomilikiwa na kanisa hilo, katika kijiji cha Masisiwe, wilayani Makete, mkoani Njombe jana. **PICHA: OMR**

# Tulia Rais mpya IPU, aanika mikakati yake

**Na Romana Mallya**

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amechaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) katika uchaguzi uliofanyika jana jijini Luanda, Angola.

Baada ya ushindi huo, mwenyewe ameweka wazi mikakati yake ukiwamo wa kuhakikisha nchi ambazo hazina amani, watahakikisha inarejea kwa kushauri serikali zake kujiepusha na mambo ya kivita na kuzisimamia ili nchi zisiendelee kuingia katika vita.

Katika uchaguzi huo uliofanyika jana, Dk. Tulia alishinda kwa kupata kura 172 kati ya 303 zilizopigwa, akichukua mikoba ya Rais aliyemaliza muda wake, Duarte Pacheco kutoka Ureno.

Wagombea wengine walioshiriki uchaguzi huo ni Catherine Hara kutoka Malawi aliyepata kura 61, Adji Diarra kutoka Senegal kura 51 na Marwa Hagi kutoka Somalia aliyepata kura 11.

Baada ya kutangazwa mshindi, Dk. Tulia alisema kuwa hiyo ni nafasi kubwa kwa Tanzania kuonekana zaidi duniani, akiahidi kutangaza amani duniani.

"Nimefurahi sana kupata nafasi hii, ni heshima kubwa kwa nchi yetu ya Tanzania kwa mwanamke kushika nafasi hii. Nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa heshima kubwa ambayo ameiletea nchi yetu kwa maana kwamba yeye ndiye aliyekubali mimi nigombee nafasi hii.

"Nitumie nafasi hii kumshukuru sana kwa heshima hii kubwa ambayo kwa yeye kuturuhusu kugombea nafasi hii, ameliletea taifa letu heshima kubwa na sasa tumepata nafasi kuongoza Jumuiya ya Mabunge Duniani," alisema.

Dk. Tulia alisema kwa sasa nafasi hiyo imeipa Tanzania na ni wakati wa nchi kuonekana nje.

Kuhusu namna alivyojipanga katika nafasi hiyo mpya kwake, Dk. Tulia alisema itamchukua muda kidogo kwa ajili ya kujifunza kazi za taasisi hiyo.

Kwa ujumla, Dk. Tulia alisema kuna mambo ameshaahidi kipindi cha kampeni, hivyo ataanza nayo.

"Mojawapo ni kuhakikisha kwamba katika mazingira haya tuliyonayo, sehemu nyingi zina vita, hivyo nitahakikisha kama Jumuiya ya Mabunge Duniani, sehemu nyingine ambako hakuna amani, tunapeleka amani kwa maana ya kushauri serikali zetu kujiepusha na mambo ya kivita na kuzisimamia serikali zetu ili nchi zisiendelee kuingia katika vita," alisema.

Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Mussa Zungu, alimpongeza Dk. Tulia kwa hatua hiyo na kumtakia mafanikio katika majukumu yake mapya.

Zungu alisema kwa sasa Dk. Tulia anakuwa na majukumu ya kusimamia amani, demokrasia na kuendeleza miradi yote itakayokuja nchini.

Pia ana jukumu la kuhakikisha wanawake wanapata nafasi kubwa katika siasa na nchi zote kuheshimu sheria za kimataifa ili kusimamia amani.

"Tunampongeza Dk. Tulia, amefanya kazi kubwa, timu ya Tanzania imefanya kazi kubwa sana, lakini yote Mwenyezi Mungu amesaidia na kutupa ushindi huu, na pongezi hizi ni za Mama Samia," alisema.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema kazi kubwa ambayo Dk. Tulia anakwenda kuifanya ni kuhakikisha anaimarisha uhusiano bora wa nchi zote duniani. Amemtakia heri katika kazi zilizo mbele yake.

Mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu, alisema heshima iliyowekwa na Dk. Tulia katika uchaguzi huo kwa kushinda dhidi ya wapinzani wake ni matokeo ya jitihada zilizokwewa na Rais Samia katika kujenga na kuimarisha uhusiano na mataifa mengi duniani.

# RC Chalamila aahidi wawekezaji tatizo la umeme kuisha karibuni

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amewahakikishia wafanyabiashara na wenye viwanda kuwa tatizo la kukatika kwa umeme litaisha hivi karibuni.

Amesema tatizo hilo litakwisha kutokana na mikakati kabambe iliyofanywa na serikali ikiwamo kutafuta vyanzo vipya vya nishati hiyo.

Katika mkutano na wanachama wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI) jana, Chalamila alisema anafahamu changamoto kubwa ya umeme ambayo wafanyabiashara hao wanapitia kutokana na kukatika umeme mara kwa mara.

Alisema serikali imesimama imara kuweka mipango ambayo itaondoa hali hiyo kwa muda mrefu.

Kiongozi huyo alisema ukame uliopita ulipunguza kiwango cha maji, hivyo kupunguza uzalishaji umeme kwa njia ya maji. Sababu nyingine ni ongezeko la watumiaji wa nishati hiyo.

"Watumiaji wa umeme wamekuwa wengi, lakini umeme ni uleule, ndiyo maana serikali inafanya jitihada kupata vyanzo vingi na kuna Bwawa la Mwalimu Nyerere kule Rufiji, umeme utakaozalishwa ni MW 2,115, kuna mradi wa Rusumo, kwahiyo ndani ya muda mfupi ujao, hali itakuwa nzuri," aliahidi.

Chalamila alisema Mkoa wa Dar es Salaam kwa sasa hauna shida ya maji kwa kuwa mahitaji ya kila siku ni lita milioni 544, lakini uzalishaji wake ni lita milioni 590, hivyo kuna ziada ya uzalishaji.

Alisema tatizo lililopo ni kasi ya mamlaka husika kuunganishia wananchi huduma hiyo. Baada ya ukame wa mwaka jana, serikali ilichimba visima tisa. Mpaka sasa, visima sita vinafanya kazi na tayari tanki lenye uwezo wa kubeba lita milioni sita limeshajengwa.

"Upande wa maji kilichobaki ni kuharakisha mtandao wa maji uwafikie wananchi wengi, jambo lingine ambalo Rais (Samia Suluhu Hassan) amelifanya ni kuwekeza kwenye Bwawa la Kidunda ambalo litaleta maji Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, lakini na ninyi kwenye shughuli zenu muwe mnafikiria suala la mazingira, kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Mkurugenzi wa CTI, Leodegar Tenga, aliomba serikali kupunguza utitiri wa tozo za magari ya wafanyabaishara kuingiza bidhaa katikati ya mji kwa kuwa zinaongeza gharama za uzalishaji.

Alisema wenye viwanda wanatengeneza bidhaa ambazo wanalazimika kuzisambaza maeneo ya mijini, lakini ili magari yao yafike huko yanalazimika kutoa tozo zinazoanzia Sh. 20,000 kwa magari madogo na ya ukubwa wa kati Sh. 50,000 kwa siku au Sh. 200,000 kwa mwezi.

"Hii inasikitisha sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa sababu hakuna mtu anayeweza kuzalisha bidhaa asizipeleke mjini, lakini anapozipeleka anaadhibiwa kwa kutozwa tozo nyingi. Kwahiyo, tunaomba serikali iliangalie maana ni kilio cha muda mrefu," alisema.

Tenga pia aliiomba serikali itengeneze mifereji ya kuchukua maji wakati mvua zinaponyesha kwa kuwa kwenye maeneo ya Chang'ombe, hali huwa mbaya wakati wa mvua za masika.

"Barabara zile huwa zinaharibika sana kwa sababu hakuna mitaro na msongamano wa magari unakuwa mkubwa sana, tunaomba TARURA (Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini) wafanye jambo kupunguza usumbufu huu," alisema.

Tenga pia alisema kwenye maeneo ya viwanda kumezuka Bandari Kavu (ICD) nyingi, hali ambayo imesababisha msongamano mkubwa wa magari mengi makubwa kiasi kwamba wenye viwanda wanakosa fursa ya kufanya shughuli zao.

Alisema magari yanayoingiza kwenye ICD hizo wakati mwingine huziba barabara na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wenye viwanda.




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, akimnadi mgombea wa kiti cha Uwakilishi jimbo la Mtambwe kupitia chama hicho, Mohamed Ali Suleiman, katika mkutano wa kufunga kampeni huko Daya Mtambwe Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

HARUFU YA RUSHWA

# Bati moja lanunuliwa kwa 43,000/- mradi wa serikali

## •TAKUKURU yashtukia mchezo mchafu

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida imeokoa Sh. milioni 54.088 zilizotokana na wazabuni kutowasilisha Kodi ya Zuio katika Mamlaka ya Mapato (TRA) na kupeleka vifaa pungufu kwenye miradi tofauti ya maendeleo.

Miongoni mwa 'madudu' yaliyofichuliwa na TAKUKURU ni bati moja kuuzwa kwa Sh. 43,000/- katika mradi wa ujenzi wa shule.

Akitoa taarifa ya kipindi cha miezi mitatu ya Julai-Septemba mwaka huu, Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Sipha Mwanjala alisema katika kipindi hicho walifuatilia utekelezaji wa miradi 13 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.627 kwenye sekta za elimu na barabara.

Alisema kiasi hicho cha fedha pia kinajumuisha miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na fedha za serikali kuu zilizoelekezwa mkoani Singida kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

Kati yake, zimo fedha za miradi mitatu yenye thamani ya Sh. bilioni 1.48 ambayo ilikutwa na upungufu mbalimbali na ushauri ulitolewa ili kukabiliana nao.

Kwa mujibu wa Sipha, miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Shule ya Msingi ya Mnung'una iliyoko Manispaa ya Singida, ujenzi wa Shule ya Msingi Ikyeto iliyoko wilayani Iramba na ujenzi wa shule mpya ya awali na msingi Nkindiko.

Sipha alibainisha kuwa kutokana na ufuatiliaji wa miradi uliofanyika, taasisi hiyo imeokoa Sh. milioni 54.088 zilizotokana na kutowasilishwa Kodi ya Zuio TRA na wazabuni kupeleka vifaa pungufu katika miradi tofauti na madai aliyowasilisha au feha alizolipwa.

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alibainisha zilizookolewa pia zinajumuisha za ujenzi wa shule mpya ya Nyerere iliyoko Manispaa ya Singida kupitia uzuiaji rushwa Sh. milioni 8.256 katika ununuzi wa mabati 192 ambayo kila moja liliuzwa kwa bei ya Sh. 43,000, gharama ya venti za juu ya milango 16 ambazo ziliuzwa kwa Sh. 20,000 na hivyo kufanya jumla ya Sh. 320,000.

Miradi mingine ni ya ujenzi wa Shule mpya ya Manga Manispaa ya Singida ambao jumla ya Sh. 306,000 zilikuwa zimetengwa kununua gypsum board 17 kwa bei ya Sh. 18,000, Sh. 610,000 za gharama ya madawati 10, ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu manne ya vyoo pamoja na vanishi ya madawati 50.

"Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Wembere iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi (Sh. milioni 21.356, Shule ya Msingi Mtavira Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi (Sh. milioni 3.979) Singida DC (Sh. milioni 4.725) pamoja na Singida Manispaa Sh. 14.535 na hivyo kufanya jumla ya Sh. milioni 54.088," alifafanua Kaimu Mkuu wa TAKUKURU.

Alisema taasisi hiyo iliendeleza na utekelezaji wa Programu ya TAKUKURU RAFIKI kwa kufanya vikao 18 na wadau katika kata 18. Huko wadau waliibua kero 175 na kati yake, zilizotatuliwa mpaka sasa ni 125, wanaendelea kuzitafutia ufumbuzi kero 50.

**CAG, WATAALAMU**

Ripoti ya Uwajibikaji ya Viashiria vya Rushwa, Ubadhirifu na Udanganyifu 2021/22 iliyoandaliwa na Taasisi ya WAJIBU kutokana na ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za ukaguzi wa Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Mamlaka ya Serikali za Mitaa za mwaka wa fedha 2021/22, zinabainisha miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya uwajibikaji, kiasi ambacho aidha hakikukusanywa au kimetumiwa na serikali pasipo kupata tija yoyote (nugatory expenditure) kimepungua kwa asilimia 33 kutoka Sh. bilioni 4,590.73 kwa mwaka wa fedha 2020/21, hadi Sh. bilioni 3,084.55 kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Vilevile, uchambuzi umebaini kuwa Mashirika ya Umma yamekuwa na ongezeko la asilimia 43 ya jumla ya miamala ambayo inaviashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu kutoka Sh. bilioni 1,408.36 mwaka wa fedha 2020/21 hadi Sh. bilioni 2,015.78 mwaka wa fedha 2021/22.

"Jumla ya miamala yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika Mashirika ya Umma pekee ni Sh. bilioni 2,015.78 sawa na asilimia 65 ya jumla ya miamala yote yenye viashiria vya rushwa ubadhirifu na udanganyifu ya Sh. bilioni 3,084.55 kwa mwaka wa fedha 2021/22," Taasisi ya WAJIBU inabainisha katika uchambuzi wake huo.

# Mbaroni madai kusababisha kifo cha msaidizi wa ndani

**Na Mary Mosha,** HAI

JESHI la Polisi Mkoa wa Kilimanjaro linamshikilia mtuhumiwa mwanamume (jina linahifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi) kwa tuhuma za kusababisha kifo cha msaidizi wa ndani, Zuwena Bihumo (14) mwenyeji wa Kigoma.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Simon Maigwa, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Oktoba 23 mwaka huu katika Kijiji cha Uswaa, Wilaya ya Hai.

Alisema kifo cha binti huyo kinadaiwa kutokea baada ya mtuhumiwa huyo na mke wake kumfanyia ukatili binti huyo kwa kumchapa na kitu kinachodhaniwa ni fimbo maeneo mbalimbali ya mwili wake na kumsababishia majeraha makubwa yaliyosababisha kifo chake.

"Baada ya kutenda unyama huo, waajiri hao walimfikisha binti huyo Hospitali ya Wilaya ya Hai kama mgonjwa huku wakitambua kuwa alishafariki dunia muda mrefu," alidai Kamanda Maigwa.

Jeshi hilo pia limemkamata Semeni Halfani (45), mkazi wa Kitongoji cha Reli Juu wilayani Mwanga, kwa tuhuma za kumsababishia kifo mwanawe Shamsidin Msemo (13) kwa kummwagia mafuta ya taa huku akiwa amemfunga mikono na kumchoma moto.

Kamanda Maigwa alisema baada ya juhudi za muda mrefu kwa kushirikiana na wananchi wema walifanikiwa kumkamata mama huyo Ifakara mkoani Morogoro alikokuwa amekimbilia kwa ajili ya maficho.




Alisema kuwa Agosti 31 mwaka huu, saa 11 jioni, nyumbani kwa mtuhumiwa, alimtuhumu mtoto wake huyo kuchukua viazi vya kukaanga pamoja na Sh. 20,000 bila rukhusa yake.

Alisema tuhuma hizo ndizo zilizomfanya mama huyo kumfunga kamba mtoto huyo na kummwagia mafuta ya taa kisha kumchoma moto na kumsababishia majeraha makubwa na kupelekea kifo chake kilichotokea Oktoba 3 mwaka huu wakati akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda (KCMC).

"Baada ya juhudi kubwa za muda mrefu na kushirikiana na wananchi wema, tumefanikiwa kumkamata mama huyu huko Ifakara mkoani Morogoro. Kwa sasa uchunguzi ukikamilika tutamfikisha mahakamani," alisema Kamanda Maigwa.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

KARIM M AJANI anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T 244 AKQ, CHASSIS NAMBA: TD01W203789 na ENGINE NAMBA: G16A203789. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/5061/2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 09/2023**
**(Asilia Shauri la Jinai Na. 20/2021, Mahakama ya Mkoa Mtwara)**
**MKURUGENZI WA MASHTAKA...........MRUFANI**
**DHIDI YA**
**MT.95850 CPL SHAIBU NA WENZAKE WATATU...........MJIBU RUFAA**
**KUITWA SHAURINI**
**KWA: SELEAMANI HAMIS BAISE**
**MTWARA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama kuu Mtwara kusikiliza rufaa hii mnamo tarehe 30/10/2023 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.

Kumbuka kuwa endapo hutafika mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi rufaa hii itasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 07/09/2023.

C.T.MNZAVA
KAIMU NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

# Mganga mbaroni kwa tuhuma kuua, kunyofoa sehemu za siri

**Na Vitus Audax**

WATU wawili akiwamo mganga wa kienyeji wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Geita kwa tuhuma za kumuua kisha kumnyofoa sehemu za siri Joyce Luhendeka (51) katika tukio linalohusishwa na imani za kishirikina.

Joyce, mkazi wa Kijiji cha Ikobe wilayani Mbogwe, anadaiwa kuuawa na kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali shingoni kisha kunyofolewa sehemu zake za siri, ikidaiwa zilihitajika kwa mganga wa kienyeji kwa ajili ya ramli.

Mtoto wa marehemu, Mrekwa Mpembo, alidai mama yake aliuawa Oktoba 12 mwaka huu usiku wakati akitokea katika shughuli zake za kuuza ndizi.

Alisema kuwa baada ya mauaji hayo, mwili wake ulitekelezwa kando ya shamba la mpunga karibu na nyumbani kwake.

Mpembo aliiomba serikali kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahusika wa tukio hilo ili kukomesha vitendo vya kikatili kama hivyo mkoani Geita viliko kithiri na maeneo mengine nchini.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Mshanete Mashauri, alisema kuwa baada ya kupokea taarifa hiyo, alilijulisha Jeshi la Polisi.

Alidai kuwa uchunguzi wao wa awali umebaini wahalifu hao wanadaiwa kupatiwa Sh. 300,000 kwa ajili ya kutekeleza ukatili huo. Alidai hayo ni maelekezo ya dada wa marehemu na mganga wa kienyeji ambao wanashikiliwa polisi.

Alisema Jeshi la Polisi lilifika nyumba kwa dada huyo na kukuta kiungo hicho cha siri cha marehemu kikiwa kimening'inizwa ndani ya nyumba. Mtuhumiwa anadaiwa kukiri mbele ya polisi na wananchi kuhusika na tukio hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi Safia Jongo, alisema jeshi hilo linawashikilia watu wawili ambao ni dada wa marehemu na mganga wa kienyeji ambao majina yao kwa sasa yamehifadhiwa kwa ajili ya upelelezi.

Alidai kiungo hicho kiliagizwa na mganga huyo wa kienyeji kupitia ramli chonganishi kwa kile kilichodaiwa kuwa dada huyo alimtuhumu ndugu yake (marehemu) kuhusika na kifo cha binti yake.

"Mama huyo baada ya kumtilia shaka ndugu yake kuhusika na kifo cha mwanawe, alikwenda kwa mganga wa kienyeji ambaye kupitia ramli chonganishi, alimtaka alete viungo hivyo vya siri vya huyo mama na auawe," alisema.

Kamanda huyo alisema watuhumiwa hao wanaendelea kushikiliwa na taratibu za kisheria zitafanywa huku akiwataka wananchi kuacha imani za kishirikina na kuepuka ramli chonganishi.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akizungumza wakati wa kikao cha wanachama wa Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri: Wanawake wasomi washiriki ufafiti, uchunguzi

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana, amesema wanataka kuona wanawake wasomi wengi zaidi wakishiriki katika utafiti, uandishi na uchunguzi ili kuleta mabadiliko ndani ya nchi.

Juzi jijini Dar es Salaam katika uzinduzi wa kitabu cha 'The Fatimids' kilichoandikwa na mwanazuoni Dk. Shainool Jiwa, Waziri Chana alihimiza Watanzania kujenga utamaduni wa kusoma na kuandika vitabu, akisisitiza kufanya hivyo kutaongeza ufahamu kwa kizazi kilichopo na kijacho.

Kitabu hicho kimeandikwa na mwanazuoni huyo kwa kushirikina na Mtandao wa Maendeleo wa Aghakani (AKDN) na Taasisi ya Taaluma ya Ismaili, kina maudhui ya historia ya dini ya Kiislamu na utamaduni wake.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameweka miundombinu wezeshi kwa sekta ya elimu ikiwamo utoaji wa elimu bure kuanzia shule za msingi hadi sekondari ili kuhakikisha wanapatikana wataalamu kutoka nyanja mbalimbali ikiwamo waandishi wa vitabu.

"Kwa mfano, leo (juzi) Dk. Shainool Jiwa, anazindua kitabu chake ambacho anaweza kukiuza ndani na nje ya nchi yetu. Kwahiyo, Watanzania hasa wanawake kwa ujumla changamkieni fursa ya kufanya utafiti, uchunguzi na kuandika vitabu kwa faida ya kizazi chetu," alihamasisha.

Balozi Dk. Chana alimpongeza mwandishi wa kitabu hicho kwa kuchagua mada ya kipekee inayohusiana na masuala ya dini ya Kiislamau na utamaduni wake baada ya kufanya utafiti wa kitaalamu kwa muda mrefu.

"Tunataka kuona wanawake wakishiriki kwenye nyanja mablimbali katika nchi yetu, kama vile utafiti, uandishi na uchunguzi, hizi ni

sekta ambazo huko nyuma tulikuwa hatuoni wanawake wakifanya.

"Kuandika kunasaidia kutoa ufahamu kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine, vitabu kama hivi vinaweza kutumika katika maktaba zetu shuleni, pia kama rejea. Sasa ni wakati wa wanawake wasomi kuleta mabadiliko kama ambavyo Rais anasisitiza," alihimiza.

Mwandishi wa kitabu hicho ambaye pia ni Mwanazuoni Mashuhuri na Mtafiti, Dk. Shainool alisema ameamua kuandika kitabu hicho kwa lengo la kuwapa watoto, vijana na wakubwa maarifa, ujuzi, mitazamo na maadili ya kuwasaidia kuchangamana na dunia na kuchangia katika jamii ya watu wengi.

## Mvua yawaacha bila makazi

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

WATU 150 wamebaki bila makazi baada ya nyumba 30 kuezuliwa na nyingine kubomoka kutokana na mvua kubwa iliyonyesha juzi katika Kijiji cha Kaluko, Kata ya Chitete wilayani Kalambo mkoani Rukwa.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, Mwenyekiti wa serikali ya kijiji hicho, Edwin Kasama alisema mvua hiyo ilianza kunyesha Oktoba 26 majira ya saa 10 jioni ikiambatana na upepo mkali.

Alisema kuwa ulianza upepo mkali kisha ikafuatia mvua kubwa ambapo ilisababisha kubomoka baadhi ya nyumba kijijini huko huku nyumba nyingine zikiezuliwa paa na kuziacha baadhi ya familia bila makazi.

"Baadhi ya wanakijiji nyumba zao zimebomoka kabisa, hawana hata sehemu ya kulala tena, wana watoto, hivyo tunaiomba serikali iwasaidie kwa kuwa wanapitia wakati mgumu, vitu vyao vimeharibika kabisa," alisema Kasama.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Paskalia Katata alisema mvua hiyo imewaacha katika hali mbaya kwa kuwa hawana fedha za kukarabati nyumba zao zilizoharibika, wanategemea msaada wa wahisani na serikali kwa kuwa hali zao kiuchumi si nzuri.

Diwani wa Kata ya Chitete, Patrick Benson alisema kuwa kutokana na tukio hilo, baadhi ya wananchi ambao nyumba zao zilisalimika wamejitolea kuzipa hifadhi familia ambazo makazi yao yalibomoka.

Alisema kuwa changamoto iliyopo ni namna ya kuwahudumia wananchi ambao walikumbwa na mkasa huo kwa kuwa hawana chakula na mahitaji mengine muhimu. Vitu walivyokuwa navyo viliharibika baada ya kulowa.

Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, Lazaro Komba alithibitisha hali hiyo na kuwataka wananchi wa wilaya hiyo kuhakikisha wanajenga nyumba bora zitakazohimili hali zote ikiwamo mvua yenye upepo mkali na majanga mengine.

# Mikataba ya usafirishaji gesi asilia Tanzania-Uganda yaiva

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI za Tanzania na Uganda zimekubaliana kuwa rasimu ya mkataba mahsusi baina yake katika utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania kwenda Uganda itiwe saini mwezi ujao jijini Dodoma.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga na Naibu Waziri wa Nishati wa Uganda, Peter Lokeris walikubaliana hayo wakati wa kikao cha majadiliano kuhusu ujenzi wa mradi huo kilichofanyika juzi jijini.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, Balozi wa Uganda nchini, Kanali mstaafu Fred Mwesigye, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Musa Makame na wataalamu wengine kutoka Wizara ya Nishati kwa pande zote.

Akizungumzia hatua zilizofikiwa katika majadiliano hayo, Judith alisema Wizara ya Nishati imekwishawasilisha nyaraka muhimu kwa wadau wote wanaohusika katika utekelezaji wa mradi huo ikiwamo Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Alisema wizara pia imeshapokea maoni kutoka kwa wadau hao ambapo tayari Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameridhia kuendelea na hatua zinazofuata.

Naibu Waziri wa Nishati wa Uganda, Peter Lukeris alisema mradi huo ni muhimu kwa nchi zote mbili, hivyo ni vyema kuanza utekelezaji hatua za awali hususani kutia saini nyaraka zilizoandaliwa ikiwamo Rasimu ya Mkataba Mahsusi Baina ya Tanzania na Uganda.

Vilevile, alieleza kuwa kutiwa saini kwa mkataba huo kutawezesha shughuli zingine za utekelezaji mradi huo kuanza na kuleta manufaa kwa mataifa hayo mawili.

Awali akiwasilisha taarifa za mradi huo, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mramba, alieleza kuwa timu ya wataalamu ya pamoja iliandaa nyaraka mbalimbali ambazo ni Rasimu ya Mkataba Mahsusi Baina ya Tanzania na Uganda, Rasimu ya Kanuni za Ununuzi za Pamoja na Rasimu ya Hadidu za Rejea.

Na baada ya kuandaa nyaraka hizo, timu hiyo ya wataalamu ilikubaliana kupata maoni na idhini kutoka mamlaka zinazohusika na mradi huo kutoka nchi zote mbili na kuzifanyia kazi kwa hatua zaidi.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akifurahia jambo na Meneja Mwandamizi wa kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) anayesimamia mahusiano ya jamii, Gilbert Mworia (kushoto), alipotembelea banda la kampuni hiyo katika maonyesho yaliyokuwa yanaendelea kando ya Kongamano la Kimataifa la Uwekezaji na Madini Tanzania 2023, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chongolo amtwisha mzigo Makonda

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amewataka Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa - Itikadi na Uenezi, Paul Makonda na Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia Hamid kuanza majukumu yao wakitambua imani kubwa waliyopewa katika kutumikia chama hicho.

Akizungumza na wateule hao jana jijini Dar es Salaam, Chongolo aliwatakia heri katika majukumu yao na kuwaelekeza kuwa baada ya kukabidhiwa ofisi zao na majukumu yao rasmi na watangulizi wao, waanze kazi mara moja kwa kuwa hakuna muda wa kusubiria.

Changolo alisema nafasi hizo mbili; Idara ya Itikadi na Uenezi na Idara ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa ni za kimkakati kwa CCM, hivyo Makonda na Rabia wanapaswa kujua kuteuliwa kwao ni sehemu ya kuongeza chachu na kasi ya idara hizo kutekeleza malengo yaliyokusudiwa na CCM katika kutumikia wananchi na kuzisimamia serikali zote mbili.

"Karibuni sana. Hongereni sana kwa kuaminiwa na kuteuliwa. Ujio wenu utakuwa sehemu ya kuongeza kasi ya yale ambayo chama tumekusudia. Uenezi na siasa ndio kila kitu. Mmeaminiwa na kuteuliwa kushika maeneo muhimu.

"Siasa na Uhusiano wa Kimataifa na Itikadi na Uenezi ni mojawapo ya 'core activities' (shughuli za msingi) za siasa yetu na imani ya chama chetu.

"Hatuna shaka na ninyi. Tunatarajia mtafanya makubwa kufikia malengo. Tuna maandalizi ya uchaguzi hapa 2024 na 2025. Tuko kwenye reli… tuko kwenye njia sahihi. Karibuni sana!" alisema Chongolo.

Alieleza kuwa CCM iko salama na imara katika kusimamia misingi, shabaha na malengo yake, ikiwamo kuendelea kuwa daraja la kusikiliza na kutatua changamoto za wananchi.

Alisema hali hiyo inatokana na jinsi ambavyo chama kinaendelea kuwatumikia wananchi kwa kuzisimamia serikali zote mbili ambazo zimeendelea kutafsiri maelekezo ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya 2020-2025 kwa vitendo.

# Waziri Mkuu apongeza mgodi utekelezaji CSR

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ametembelea banda la Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) katika maonesho ya madini kando ya Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika Sekta ya Madini Tanzania (TMIF) na kuipongeza kampuni hiyo kwa kutekeleza kikamilifu Mpango wa Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR).

Majaliwa ambaye pia juzi alifunga mkutano huo kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alipata maelezo kutoka kwa Meneja Mwandamizi anayeshughulikia uhusiano wa jamii kutoka GGML, Gilbert Mworia na kupongeza kazi kubwa inayofanywa na kampuni hiyo ikiwamo kuwa mdhamini mkuu wa mkutano huo.

"Tunawapongeza sana kwa kuwa mfano wa kuigwa katika kuzingatia matakwa ya sheria ya madini kuhusu kipengele hicho cha CSR. Kwa mfano, katika hili suala la ujenzi wa uwanja wa mpira Magogo mnatakiwa kumalizia kulitekeleza haraka ndani ya miezi sita.

"Lakini pia msiangalie kujenga uwanja mkoani Geita peke yake, mpeleke huduma hizi na mikoa mingine ili ifaidike na kukuza vipaji vya vijana wetu," Majaliwa aliagiza.

Awali akitoa maelezo kwa Waziri Mkuu, meneja huyo mbali na kuelezea mikakati ya GGML katika kuhakikisha Watanzania na jamii inayozunguka mgodi inanufaika na kuwapo kwa kampuni hiyo, pia alisema kampuni hiyo imekuwa kinara katika kuzingatia masuala ya uhifadhi wa mazingira, afya na usalama mahala pa kazi.

Mworia alisema GGML imeendelea kuwa mfano wa kuigwa nchini kutokana na kuzingatia suala la afya na usalama mahala pa kazi hali iliyoifanya kampuni hiyo kushinda mara nne mfululizo tuzo hiyo inayotolewa na kampuni mama ya AngloGold Ashanti na kuishinda migodi mingine duniani.

Kuhusu ujenzi wa uwanja huo wa mpira, Mworia alimhakikishia Waziri Mkuu kuwa ndani ya miezi sita utakuwa umekamilika, lakini wataandaa mpango wa kutoa mchango katika sekta hiyo kwenye mikoa mingine.

Hata hivyo, akifunga maonesho hayo yaliyofanyika tarehe 25, 26 Oktoba mwaka huu, Majaliwa alisema serikali itaendelea kuipa umuhimu sekta ya madini ili kuwa injini ya uchumi wa Taifa.

Alisema serikali iko tayari na inaruhusu miradi ya maendeleo kutoka sekta binafsi katika utafutaji, uchimbaji, uchorongaji na uongezaji thamani madini ili kufanikisha mikakati iliyopo kwa wachimbaji kwa wachimbaji wote nchini.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde alisema wizara imetumia mkutano huo kukuza ushirikiano wa kikazi baina ya nchi na nchi kupitia mada mbalimbali zilizowasilishwa kama vile majadiliano kuhusu matumizi ya nishati safi ili kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kwa mwaka 2023, mchango wa wachimbaji katika sekta madini, serikali imeikusanya Sh. bilioni 678 sawa na asilimia 40 ya makusanyo yote, hali inayoonesha sekta hiyo imepiga hatua.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushindani mechi za Ligi Kuu usisubiri lala salama

**LIGI** Kuu Tanzania Bara inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali inaendelea kwenye viwanja tofauti hapa nchini na sasa imeingia katika raundi ya saba.

Ligi hiyo ndio inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo hufanyika kila mwaka na chini ya usimamizi wa viongozi wa Shirikisho la Soka barani hapa (CAF).

Simba maarufu Wekundu wa Msimbazi leo wanatarajia kushuka kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwakaribisha 'wababe' wa Yanga, Ihefu kutoka Mbarali mkoani Mbeya wakati keshokutwa JKT Tanzania itawavaa Dodoma Jiji FC, Prisons itawaalika Geita Gold na Tabora United ikiwafuata Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba.

Kila mechi katika ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), ni muhimu na hakuna mchezo unaotakiwa upewe kipaumbele au wachezaji kuweka umuhimu zaidi kwa sababu unaposhinda unapata pointi tatu, mnagawana pointi pale mnapotoka sare na unapofungwa unapoteza pointi zote.

Kumekuwa na hali ya kujisahau au kubweteka kwa baadhi ya timu na kutojituma katika mechi za mzunguko wa kwanza na pale zinapopoteza michezo, hali huwa mbaya na kuanza mikakati ya kujinusuru inapofika mzunguko wa pili.

Imekuwa ni kawaida kuona wadau, viongozi wa klabu na hata serikali za mikoa husika kuunganisha nguvu pale wanapoona timu yao au zao zimekalia kuti kavu au ziko kwenye hatari ya kushuka daraja kwa kuahidi kiasi cha fedha au zawadi nyingine ili kusaka ushindi.

Nipashe inawataka wadau hao kufanya mipango au mikakati hiyo sasa na kuacha tabia ya kusubiri ligi ikiwa inaelekea ukingoni kwa sababu wengi huishia kushuka daraja.

Mipango sahihi inatakiwa ifanyike sasa wakati bado Ligi Kuu Tanzania Bara iko mbichi kwa kila timu kuhakikisha inashinda michezo yake ya mzunguko wa kwanza na pale mzunguko wa lala salama unapoanza, mambo yanakuwa mepesi na si kuomba dua ya kunusurika.

Wadau wa soka wa kila klabu wanatakiwa kuwa karibu sasa na viongozi wa timu pamoja na wachezaji wao ili kusaka pointi tatu muhimu ambazo zitawaweka kwenye nafasi salama katika msimamo wa ligi hiyo ambayo sasa inashika nafasi ya saba kwa ubora Afrika.

Pia wadau hao wanatakiwa kushiriki kwa karibu katika kuangalia mapungufu ya kikosi na kupanga namna ya kukiongezea nguvu katika usajili wa dirisha dogo ambao utafunguliwa ifikapo Desemba 16, mwaka huu, kwa kufanya haya utasaidia kujiondoa katika hatari ya kushuka daraja.


Timu zinatakiwa kubadilika, kujipanga katika kila mechi lakini pia kuacha tabia ya kuchagua au kudharau baadhi ya mechi, hali hii inaleta sintofahamu na kuamsha maswali mengi ambayo mwisho wa siku hayajengi na hayasaidii katika maendeleo ya mchezo husika.

Kujipanga mapema si kwa timu za Ligi Kuu Tanzania Bara, hili pia linazihusu timu zote zinazoshiriki Ligi ya Championship, First League, Ligi Kuu Zanzibar huku timu zinazojiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake, Ligi Daraja la Kwanza la Wanawake (WFDL) na Ligi ya Mabingwa wa Mikoa kwa Wanawake (RWCL) kukamilisha maandalizi na hasa kwa kuzingatia mapungufu yaliyojitokeza katika msimu uliopita.

Ikumbukwe kufanya vyema katika ligi zote hizi, ndio msingi wa kupata wachezaji bora wa timu za taifa kwa sababu bado idadi kubwa ya nyota wanaoitwa katika timu hizo wanacheza soka la hapa ndani ambao huungana na wenzao wachache wanaosakata kandanda la kulipwa Ulaya au katika mataifa mengine ya Afrika.

Waswahili wanasema biashara asubuhi, jioni ni muda wa kufanya hesabu, hii inamaanisha kila timu ipambane kusaka pointi sasa na kuacha kusubiri dakika za lala salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba SC, Yanga ziruhusiwe kusajili wapya kuelekea CAF

Na Adam Fungamwango

**WIKI** yote hii nimekuwa nikisikia na kuona katika mitandao ya kijamii baadhi ya timu zilizoingia kwenye hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho zimeanza kufanya usajili.

Ina maana tayari zimeanza kufanya marekebisho madogo kuelekea mechi za kwanza zinazotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

Wakati baadhi ya timu zikifanya usajili kwa ajili ya kuziba mapengo kabla ya kuanza michuano hiyo, timu za Tanzania zinaweza kuanza hatua hiyo bila ya kuwa na wachezaji wapya.

Zenyewe hazitopata nafasi ya kubadilisha kutokana na kupishana kwa kipindi cha usajili.

Wakati CAF iliruhusu klabu kufanya usajili kwa kuongeza wachezaji kwa timu zilizotinga hatua ya makundi ili mradi wasizidi 20, dirisha la usajili nchini linatarajiwa kufunguliwa ifikapo Desemba 16, mwaka huu na litafungwa Januari 15, mwakani.

Ni kweli inawezekana kabisa wachezaji watakaosajiliwa kipindi hicho wanaweza kukutana na baadhi ya mechi za makundi, lakini timu zitakuwa zimeshacheza na kumaliza mzunguko wa kwanza.

Matokeo ya mechi hizo yanaweza kabisa kuifanya timu kuwa katika hali nzuri ya kufuzu kwenda robo fainali au kwenye wakati mgumu.

Simba na Yanga zinaweza kuwa katika wakati mgumu kutokana na mapungufu yaliyopo kwa sasa, hivyo hata kama wachezaji wapya wakiingia na kuwapa matokeo yanaweza yasiwabebe kutokana na kupoteza pointi kadhaa huko mwanzo kulikotokana na mapungufu.

Simba itaanza nyumbani dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast Novemba 24, mwaka huu na siku hiyo hiyo Yanga itakuwa ugenini dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria.

Mechi za raundi ya pili zitachezwa Desemba Mosi, mwaka huu kwa Simba kuvaana na Jwaneng Galaxy ya Botwana, Yanga ikiwa nyumbani kuwapokea Al Ahly ya Misri.

Desemba 8, mwaka huu ratiba inaonyesha Simba itakuwa ugenini Morocco kucheza dhidi ya wenyeji Wydad wakati Yanga pia itakuwa Ghana kucheza dhidi ya Medeama.

Hapa tu inaonyesha mpaka mzunguko wa kwanza bado Simba na Yanga zitakuwa hazijafanya usajili wowote. Na hata mechi za Desemba 19, mwaka huu kama hata zikiwa zimesajili, huenda mchakato wa vibali na Hati za Uhamisho za kimataifa (ITC) hautakiwa umekamilika.

Sheria zinasema wachezaji wanaotakiwa kucheza michuano hiyo ni lazima wawe wamesajiliwa na klabu zao kwenye ligi za ndani na kupitishwa na mashirikisho ya soka ya nchi husika.

Ukiangalia timu hizi ambazo zinaiwakilisha Tanzania kwenye michuano inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) bado zina mapungufu na zingehitaji kabisa kuongeza wachezaji wachache ili kuzifanya zicheze kwa ufanisi.

Mfano ukiiangalia Yanga ina tatizo la straika, yaani mshambuliaji wa kati. Ilihitaji mchezaji huyo kabla ya hata mechi zake za kwanza.

Simba pia ukiitazama, utagundua ina tatizo la kiungo halisi mkabaji, na hata wasaidizi wa pembeni wenye uwezo.

Hawa wote walitakiwa kupatikana kabla ya michuano hiyo kuanza kama tunavyoona baadhi ya nchi timu zikiwa zinaendelea kufanya maboresho katika vikosi vyake.

Kwa maana hiyo, ikiwapendeza na maslahi mapana ya taifa, Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na Bodi ya Ligi kuwaruhusu Simba na Yanga kusajili wachezaji kabla ya muda wa dirisha dogo kwa ajili ya mechi za CAF.

Ikiwezekana wachezaji hao wasicheze ligi kwanza mpaka kipindi cha kufunguliwa kwa dirisha dogo ili kuwe na 'fair play' kwa klabu nyingine za Ligi Kuu, lakini waidhinishwe na TFF kucheza michuano ya kimataifa iliyoko mbele yao.

Vinginevyo wachezaji hao wapya watakaowasajili wanaweza wasiwe na hawana msaada wowote katika mechi za kimataifa, kwa sababu watasajiliwa kwa fedha nyingi lakini wataishia kucheza mechi za Ligi Kuu Bara na ikiwa watabahatika kuzikuta timu zimesonga mbele sawa, lakini kama zimetolewa ni hasara na haitokuwa na maana yoyote.

## HABARI KITAIFA

KESI MAUAJI ANETH MSUYA

# Mke wa Bilionea Msuya aibua maswali, Jamhuri yaomba muda kujipanga upya

**Na Grace Gurisha**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya mauji ya Aneth Msuya umeiomba mahakama muda wa kupitia ushahidi wa Miriam Mrita, aliyekuwa mke wa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya 'Bilionea Msuya'.

Ili kupitia ushahidi wake alioutoa kwa siku nne mfululizo wiki hii, upande huo umeomba muda zaidi kwa madai kuwa ushahidi huo una mambo mengi ya kujiridhisha kwenye mamlaka husika.

Vilevile, upande wa Jamhuri uliomba ahirisho la kesi hiyo kwa siku ya jana ili utumie muda uliobaki kujiandaa na kuendelea na maswali ya dodoso kwa mshtakiwa juma lijalo. Dodoso hilo ni sehemu ya kikao cha shauri hilo.

Ombi hilo liliwasilishwa jana na Wakili wa Serikali Mwandamizi Paul Kimweri mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, baada ya mshtakiwa Miriam kumaliza kutoa ushahidi wake kwa mdomo na kwa nyaraka. Alianza kutoa ushahidi Oktoba 24 hadi jana mchana.

"Mheshimiwa Jaji, shahidi wa kwanza wa utetezi ametoa ushahidi hapa kwa siku nne kuanzia tarehe 24 hadi leo (jana), na ametoa ushahidi wa mambo mengi kwa mdomo na kwa nyaraka.

"Kwa wingi wa ushahidi wake tunahitaji kupata muda wa kupitia ili tuone tunaanzia wapi ili tupate mtiririko mzuri. Kwa sababu kuna mambo mengine aliyoyasema nyuma, lakini sasa ameyarudia na sasa hatutaki turudierudie hayo," alidai Wakili Kimweri.

Pia alidai kuwa baadhi ya vielelezo alivyovitoa mshtakiwa Miriam wanahitaji kujiridhisha na mamlaka zilizozitoa kama Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), hivyo wanahitaji muda wa kutosha ili kufanya ufuatiliaji na maandalizi ya maswali hayo.

"Kwahiyo, ni ombi letu kwamba mahakama itukubalie kuahirisha shauri hili kwa siku ya leo (jana), tuitumie na muda wote uliobaki kujiandaa na tuweze kuendelea na maswali ya dodoso katika wiki inayokuja ambayo pia ni sehemu ya kikao hiki cha shauri hili," alidai.

Baada ya Kimweri kuwasilisha ombilo hilo mahakamani, Jaji Kakolaki aliwauliza mawakili wa upande wa utetezi kuhusiana na hoja iliyotolewa ya ahirisho. Wakili Peter Kibatala na Nehemiah Nkoko walidai kutokuwa na pingamizi.

"Basi kwa kuwa upande wa mashtaka wamesema wanahitaji muda kujiandaa, na kwa kuwa maombi hayo hayakupingwa, mahakama inayakubali na ninaahirisha shauri hili hadi Jumatatu Oktoba 30, 2023 saa 3:00 asubuhi," alisema Jaji Kakolaki.

Awali, Miriam wakati anawasilisha ushahidi wake kwa kuongozwa na Wakili Kibatala, alidai kuwa ilikuwa muhimu kwa Ndeshukurwa (mama wa marehemu Aneth) kuitwa kama shahidi upande wa mashtaka kwa kuwa kama Jeshi la Polisi lilishindwa kumtafuta hadi mama wa nyumbani ndio anatoa taarifa, alitakiwa atoe ushahidi wake.

Pia alidai kuwa katika ushahidi wa dada wa kazi wa Aneth, Getruda Mfuru, kuna madai kwamba alimsikia yeye akizungumza na mshtakiwa wa pili Revocatus Muyela kilugha wakati alipokwenda nyumbani kwa Aneth.

"Mimi ninafahamu lugha ya Kipare, Kiswahili na Kiingereza kidogo na sina lugha nyingine zaidi ya hizo, kuhusiana na kwamba nilimtishia sielewi hicho kitisho kinachukua muda gani, sababu kama nilimtishia tarehe hiyo nikaondoka akabaki na bosi wake ambaye alisema alikuwa anaishi naye vizuri, akashindwa kumwambia. "Baadaye akatoka akaenda Chanika kwa rafiki yake Sabri Kombo, bado akashindwa kumwambia, alikaa siku tatu, akaenda kwa dada yake Gongolamboto, naye akashindwa kumwambia, baadaye akapewa nauli akaenda Moshi kwa wazazi wake, nako akashindwa kutoa taarifa, sielewi ni kitu gani kilikuwa kinazunguka hapa," alidai. Pia alidai kuwa Getruda alishindwa kutoa taarifa kwa mama na baba yake Aneth ambao alidai alikuwa anafanya kazi kwao.

"Na wakati huo mimi ambaye nilimtishia sipo na katika ushahidi wake alisema Mirerani alikaa na ndugu zake Aneth Natujwa, Happy, nao alishindwa kuwapa taarifa kuwa kuna kitu kinaendelea na alisema Natujwa ndiye aliyemsafirisha kutoka Mirerani kwenda kwa Aneth, naye alishindwa kumpa taarifa na wakati huo ninayemtishia sipo.

"Lakini alipopigiwa simu na Ndeshukurwa akaenda kutoa maelezo hayo polisi. Kwanini mwanzo aliogopa kutoa taarifa polisi lakini Ndeshukurwa alipowapigia simu akaenda kama hakuna kitu kilichojificha hapo ni nini?" alihoji.

Alidai kuwa Getruda siyo mtoto, ni mtu mzima mwenye watoto watatu na amesoma hadi kidato cha nne, ana elimu, lakini aliposhauriwa na Sabri kwenda polisi alikataa.

"Msichana wa kidato cha nne, amekaa kwa Aneth miezi mitano, amesema hajui chumba alichokuwa analala wala nyumba ina vyumba vingapi, ndio maana ninasema kuna kitu kimejificha hapo," alidai.

"Alipoulizwa na Wakili Nehemiah hapa, alisema yeye ndiye alikuwa mwangalizi wa nyumba na mazingira yote ya nje na kwamba hata sare yeye ndiye alikuwa anamvalisha mtoto, lakini akasema hajui zilikuwa ni sare gani, hii haiingii akilini," aliendelea kudai.

Kuhusu suala la kufanyiwa gwaride la utambuzi, Miriam alidai hakufanyiwa gwaride la utambuzi na hoja kwamb alipelekwa kwa mlinzi wa amani na akakiri kosa, haina ukweli.

Miriam ambaye ni mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya mauaji hayo ya wifi yake huyo Aneth aliyeuawa Mei 25, 2016 kwa kuchinjwa shingoni nyumbani kwake Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa kukiri kuhusika na mauaji hayo katika maelezo yake ya onyo.

Mshitakiwa wa pili ni Revocatus Muyela, wote wakazi wa Mkoa wa Arusha.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (kushoto), akijadiliana jambo na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Faru Graphite Corporation Ltd, Alimiya Osman (kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni hiyo, John De Vries, walipokutana katika Kongamano la Madini na Uwekezaji Tanzania 2023, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muhimbili kufanya upasuaji wa kwanza kupunguza uzito

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mlongazila leo inatarajia kufanya upasuaji wa kwanza wa kupunguza uzito kwa wagonjwa watano kwa njia ya kisasa.

Upasuaji huo unafanyika kwa kuingiza kamera tumboni na kupunguza ukubwa wa tumbo kwa kulishona huku faida zikitajwa ni pamoja na kumwondolea mtu uwezekano wa kupata magonjwa yasiyoambukiza na mwanawake mwenye unene kupitiliza kupata mtoto.

Mkurugenzi Msaizidi wa Huduma za Upasuaji hospitalini huko, Dk. Godlove Mfuko, alibainisha hayo juzi, akieleza kuwa huduma hiyo inaanza leo kutolewa kwa wagonjwa watano."Tunatarajia kufanya operesheni hii kesho (leo) na wagonjwa watalazwa kuanzia leo (jana) hapa hospitalini. Kila kitu kiko tayari na maandalizi yote yamekamilika na tutawafanyia wagonjwa watano.

"Faida ya operesheni hii, inafanyika siku hiyohiyo na mgonjwa hahitaji kulazwa, tumeweka siku kama tatu mgonjwa anaweza kukaa hospitalini kwa sababu mgonjwa anaweza kupatwa na lolote, ni kama vile operesheni zingine," alisema.

Dk. Mfuko alisema kuna wagonjwa watakaa siku moja na wengine wataruhusiwa siku hiyohiyo baada ya operesheni.

Alisema faida zake ni kwamba, ina uwezo wa kupunguza uzito wa mgonjwa kwa asilimia 20 mpaka 30 ndani ya mwaka mmoja.

Pia alisema huduma hiyo inasaidia kumwondolea mgonjwa madhara ya magonjwa yasiyoambukiza kama presha na kisukari.

"Mtu atakuwa na uwezo mzuri wa kukidhibiti kisukari chake, kudhibiti kiwango cha sukari kwenye damu, watu wakiwa wanene sana wanaweza kuumwa magoti, wanaweza kuvimba miguu, wengine kuumwa migongo. Kwa operesheni hii, vitu vyote hivi vinapungua katika mwili wa mtu," alisema.

Dk. Mfuko alisema utafiti unaonesha wanawake wanene sana wanaotaka kushika ujauzito, wanapopungua wanaweza kupata mimba.

"Huduma hii tunaifanya kwa mara ya kwanza na tuna mpango kazi tayari, tuna mkakati wa kuifanya iwe endelevu. Wataalamu wetu watajengewa uwezo wa kuitoa huduma hii, tutakuwa tunaweka kambi za kufanya huduma hizi kama operesheni zingine.

"Na tutapata ushuhuda kutoa kwa wateja watakaokuwa tayari kushuhudia namna maisha yatakavyobadilika kwa kuwa, hizi operesheni zinabadilisha mpaka mwonekano wa mtu na vitu vingine nilivyoeleza," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Manispaa yatenga fungu tahadhari mvua El-Nino

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imetenga Sh. milioni 30 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24 kwa ajili ya tahadhari ya mvua ya El-Nino inayotarajiwa kunyesha kuanzia mwishoni mwa mwezi huu.

Kwa mujibu wa uongozi wa halmashauri hiyo, fedha hizo zitasaidia katika ununuzi wa dawa na vyakula kwa waathirika. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Ally Machela, alibainisha hayo jana, akisema kuwa fedha hizo zitawasaidia wananchi ambao huenda wakakumbwa na mafuriko na kukosa vyakula na kupata madhara kiafya.

Machela alisema mafuriko yanapotokea mara nyingi huambatana na magonjwa kama vile kipindupindu. Tayari wameshapeleka dawa kwenye zahanati na kufungua Kituo cha Afya Lukobe ili kusaidia kupata matibabu wakazi wa kata hiyo na kata jirani.

Alisema tayari wameshatembelea wakazi wa Kata za Maghorofani, Mkundi, Kihonda na Lukobe ambazo mara kwa mara zimekuwa zikipata mafuriko na athari zake na kuwapa elimu ya namna ya kujilinda ikiwamo kuondoa mapema katika makazi yao na kutafuta maeneo mengine kabla mvua hazijaanza.

Alisema tayari manispaa imeshaanza kutengeneza barabara na miundombinu mingine ikiwamo umeme na maji katika eneo hilo la Kiegeya ambalo wananchi hao wanapaswa kuhamia.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Rebecca Nsemwa aliwataka madiwani wa manispaa hiyo kutoa elimu ya kutosha kwa wakazi wa maeneo yao kuhusu mvua ya El-Nino na namna ya kujikinga na mafuriko ikiwamo kuhama mabondeni.

Nsemwa aliwasisitiza wananchi kujenga tabia ya kuhifadhi mazingira kwa kutotupa taka kwenye mitaro inayosafishwa mara kwa mara na manispaa, sababu kubwa ikiwa ni uchafuzi unaosababisha maji kushindwa kupita na kuleta athari mbalimbali wakati wa mafuriko.




Mkurugenzi wa Biashara wa Halotel, Abdallah Salum (katikati), akikabidhi msaada wa samani za ofisini kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Oysterbay, Egidius Mjunangoma (kushoto), shuleni hapo, Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka nane ya kutoa huduma za mawasiliano nchini. Wengine ni baadhi ya walimu na wanafunzi wa shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 12/- kujenga kituo kusaidia waathirika ukatili

**Na Frank Monyo**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Msichana Initiative limesema katika mpango wake wa miaka mitano, linatarajia kujenga kituo cha kuhifadhi na kusaidia wasichana na watoto ambao ni waathirika wa ukatili wa kijinsia kwa gharama ya Dola za kimarekani milioni tano (Sh. bilioni 12.4).

Jana mkoani Dar es Salaam, Mkurungenzi Mtendaji wa shirika hilo, Rebecca Gyumi, alibainisha dhamira yao hiyo wakati wa uzinduzi wa mpango huo wa ujenzi.

Alisema dira hiyo kwa miaka mitano ijayo inalenga kudumisha mbinu zao za kuimarisha nguvu ya wasichana na kufikia zaidi ya wasichana 35,000 moja kwa moja na milioni moja kwa njia zingine kama vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ifikapo mwaka 2027.

Alisema kuwa kwa sasa nchini kuna uhaba wa nyumba salama za kuishi wasichana au watoto wanaopitia ukatili wa jinsia hivyo, wameona ni vyema kujenga kituo hicho.

"Katika dira ya miaka mitano tumepanga kutanua wigo wa matokeo yetu kupitia kujenga Kituo cha Msichana, eneo lenye sehemu nyingi ambalo litatoa sehemu salama, huduma za kisheria na kisaikolojia kwa manusura wa unyanyasaji wa kijinsia," alisema.

Rebecca alisema kuwa kituo hicho kitakuwa sehemu salama ambayo itatoa huduma za kisheria na kisaikolojia kwa manusura wa unyanyasaji wa kijinsia.

"Kwa sasa wasichana hawa hawana mahali salama pa kuishi hata kama haki itakuwa imetendeka.... wanaofanya vitendo vya ukatili hupata adhabu ya miaka 30 au zaidi jela, lakini msichana huyu anakuwa hayuko kwenye mazingira salama," alifafanua.

Rebecca alisema kuwa mkakati wao wa pili katika mpango huo unalenga kufikia mikoa minne na kufanya kazi katika kata nyingi zaidi ili kuleta tija na mabadiliko katika kupigania haki za msichana na mtoto wa kike nchini na kuimarisha nguvu na sauti zao na uongozi.

Alisema mikoa itakayofikiwa ni ya Tabora, Dodoma, Pwani na Dar es Salaam kutokana na kuwapo vitendo vingi vya ukatili na katika kufikia malengo hayo, wanahitaji Sh. bilioni 14.

"Tunalenga kubadili utamaduni wa mazoea unaorudisha nyuma haki ya mtoto wa kike, kuongeza uchechemuzi wa sera na sheria ili mifumo isiyo rasmi iimarishwe pamoja na kuimarisha taasisi yetu kwa kufikia wasichana 35,000 moja kwa moja na wasichana milioni moja kwa njia mbalimbali ifikapo mwaka 2027," alisema Rebecca.

Mkurugenzi huyo alitaja mafanikio ya mkakati wa kwanza uliomalizika mwaka 2022, yanajumuisha kuanzisha klabu za amani zaidi ya 50 ambazo zimewafikia wasichana 3,000 na zimekuwa zinashughulikia ukatili na kukuza usalama.

Alisema katika mradi wa Gape wamewezesha wasichana 301 kiuchumi na mradi wa baiskeli kwa wasichana ambao umewezesha wasichana 500 kuendelea na masomo na wale waliopata mimba kurudi shuleni. "Tumefanikiwa kuleta uchechemuzi katika sera na sheria hususan ya kubadilishwa sheria ya ndoa kuepusha ndoa za utotoni, mmeona kumekuwa na vuguvugu nchini la kubadilishwa sheria ya ndoa, tunaamini litafanyiwa kazi," alisema.

Aliongeza kuwa katika mradi wa Msichana Kafee umewezesha kutungwa kwa sheria ndogo kwa ngazi ya kata ili kulinda haki za wasichana sambamba na kuratibu kesi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Msichana Initiative, Prof. Bertha Koda alisema serikali imefanya jitihada kubwa katika kuchangia shughuli zao na kutatua changamoto za wasichana ikiwamo kubadilisha mitaala ya elimu na kutunga sera inayoruhusu mwanafunzi aliyepata mimba kurejea shuleni kuendelea na masomo baada ya kujifungua.

## Halotel yatoa msaada wa samani shuleni

**Na Zuwena Shame**

RIPOTI ya Ukaguzi Maalum wa Miundombinu na Samani za Shule za Msingi Tanzania ya Machi 2017 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ilibainisha hali mbaya kwa shule za serikali.

Shule nyingi zilibainika kuwa na uhaba wa miundombinu na samani huku miundombinu michache iliyopo ikiwa na uchakavu mkubwa.

Kukabiliana na shida hiyo, katika kuandhimisha miaka minane tangu kuanzishwa kwake, Kampuni ya Mawasiliano ya Halotel Tanzania imetoa msaada wa viti na meza kwa Shule ya Msingi Oysterbay jijini Dar es Salaam.

Wakati wa ghafla ya kutoa msaada huo jana, Mkurugenzi wa Biashara wa Halotel, Abdallah Salum, alisema kampuni imeweka mikakati ya kusaidia elimu nchini na ni moja ya uwajibikaji wake kwa jamii.

Salum alisem kuwa mchango huo ni uthibitisho wa dhamira ya Halotel iliyojikita kwenye kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu nchini na lengo lake ni kuboresha mazingira ya kufundishia kwa walimu wa shule za msingi.

"Jitihada za Halotel kwenye kurudisha kwa jamii daima zimejikita katika kuchangia kuboresha sekta ya elimu na nyinginezo nchini.

'Kwa kutoa viti na meza bora kwa walimu, kampuni inalenga kutengeneza mazingira yanayofaa kwa ufundishaji wenye ufanisi na hivyo kuwa na athari chanya katika uzoefu wa kujifunza," alisema Salum.

Salum alisema kuwa mchango huo ni muhimu kwa kuwa unaendana na jitihada za serikali kuongeza ubora wa elimu katika shule za msingi na sekondari.

Aliongeza kuwa serikali pia imejikita kwenye jukumu muhimu la kuwekeza kwenye uboreshaji mazingira ya kufundishia katika kuchochea utamaduni wa kujifunza na kupata mafanikio kwa wanafunzi.

Mkuu wa Shule ya Msingi Oysterbay, Egidius Mjunangoma alisema msaada huo ni muhimu kwa shule hiyo na kuziomba kampuni zingine ziige mfano wa Halotel kuisaidia jamii kwenye suala la elimu.

"Tunashukuru sana Halotel kwa mchango wao mkubwa katika shule yetu. Msaada huu utaboresha sana mazingira ya walimu wetu ikiwa ni pamoja na ufundishaji katika shule yetu.

"Hatua hii inaonesha dhamira ya Halotel katika kuboresha elimu na tunapongeza kujitolea kwao katika kuleta athari chanya kwenye maisha ya wanafunzi na walimu wetu shuleni," alisema Mjunangoma.

Aliongeza kuwa ni faraja kuona sekta binafsi ikishiriki kikamilifu katika kuboresha mzingira ya kujifunzia na kufundishia na wanatarajia jitihada za ushirikiano zaidi baadaye.

Shule ya Msingi Oysterbay ni moja kati ya shule nyingi za msingi na sekondari zilizonufaika na Mpango wa Uwajibikaji Kijamii wa Kampuni ya Halotel.



## Wataka kuharakishwa mfuko maalum watu wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Idara ya Vijana Taifa, Chama cha Wazazi Wenye Watoto Wenye Vichwa Vikubwa na Mgongo Wazi (ASBAHT), ameiomba serikali kuharakisha utekelezaji mfuko maalum wa watu wenye ulemavu.

Lengo ni kusaidia kupata mahitaji yao muhimu kama vile, vifaa saidizi, ruzuku kwa vyama na kuwezesha utafiti mbalimbali.

Pia ameiomba kuharakisha mchakato wa upatikanaji bima ya afya ili kusaidia upatikanaji huduma za afya kwa watu wenye ulemavu nchini.

Johari Mashaka alitoa rai hiyo juzi jijini hapa wakati akisoma risala yao katika maadhimisho ya Siku ya Ulemavu wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi.

Alisema wanaiomba serikali kutekeleza mfuko huo na kuwatambua wazazi wa watoto wenye ulemavu kama makundi maalum na kupatiwa mikopo itakayowapunguzia madhara ya unyanyasaji, unyanyapaa na ubaguzi uliojengeka miongoni mwa jamii.

"Serikali pia ifafanue kwa kina matibabu ya bure kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano kuwa ni kwa hospitali zipi? Na matibabu gani? Kwani mpaka sasa hakuna mtoto (mwenye matatizo hayo) kwenye hospitali za kibingwa anayetibiwa bure," alisema.

Johari pia aliomba hospitali zinazotoa tiba kwa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi kuongeza wigo wa madaktari na vifaa tiba ili wafikishe huduma hizo kwa jamii.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, akizungumza katika maadhimisho hayo, alisema serikali imejipanga kuhakikisha watoto wanaozaliwa na tatizo hilo, wanatibiwa na kupatiwa vifaa saidizi kupitia hospitali zote zikiwamo za mashirika na wafadhili ambao wamejitoa kuwahudumia.

Shekimweri pia aliitaka jamii kuondokana na dhana potofu ya kufikiri kuwa familia zenye watoto wenye ulemavu huo wa vichwa vikubwa na mgongo wazi zina mkosi au laana.

"Ugonjwa huu si laana wala mkosi, bali ni ugonjwa kama ilivyo kwa magonjwa mengine, hivyo hakuna sababu ya kunyanyapaa na kuwatenga, kwa kuwa unatibika kama vile kwa magonjwa mengineyo,"alisema.

Aliwataka wazazi wenye watoto walemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, kuacha tabia ya kwenda kwa waganga wa kienyeji kutafuta matibabu kwa kizingizio cha kuwa wamerogwa.

"Mtapoteza fedha zenu na mali, ugonjwa huu msije mkafikiri kama ni laana na mikosi, huo ni sawa na ugonjwa mwingine na unatibika," alisisitiza.

# Wizara yatamba ina fungu kubwa kusomesha wataalamu vifaa tiba

## Yataja kozi zenye uhakika wa ajira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imesema zipo fedha za kutosha kwa ajili ya kusomesha wataalamu wa vifaa tiba kutokana na kada hiyo kukabiliwa na uhitaji mkubwa wa wataalamu hao.

Mkurugenzi wa Mafunzo na Rasilimali Watu wa Wizara hiyo, Dk. Saitore Laizer, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati wa hafla ya kupokea Kituo cha Urekebishaji na Mafunzo ya Vifaa Tiba kilichojengwa katika Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe.

Kituo hicho kimejengwa kupitia mradi wa HPSS Tuimarishe Afya unaofadhiliwa na Serikali ya Uswisi.

Dk. Laizer alisema Watanzania wengi hawajui baadhi ya taaluma zenye mashiko ikiwamo uhandisi wa vifaa tiba kuwa hapa nchini ni eneo kubwa la kipaumbele.

"Nitoe wito kwa wanafunzi wanaomaliza kwenye shule za sekondari, wenye sifa wachangamkie kusoma katika taaluma hii.

"Miaka 12 iliyopita walipoanza kutekeleza mradi huu, wahandisi wa vifaa tiba nchini walikuwa 14. Nchi hii ni kubwa kijiografia, ina watu wengi, ina vituo vingi vya kutolea huduma za afya na vifaa tunaendelea kununua kila mwaka.

"Mashine kama CT-SCAN, sasa hivi kila Hospitali ya Rufani za Mkoa inayo na MRI zipo za kumwaga, tunahitaji wataalamu wa kutosha ambao watakaa kuanzia ngazi ya afya ya msingi hadi taifa.

"Nitoe ahadi kwa niaba ya wizara, wale wote wenye shahada ya kwanza na kuendelea ambao watapenda kujiendeleza katika eneo hili la uhandisi wa vifaa tiba, serikali itawashika mkono," alisema.

Laizer alisema eneo hilo ni la kipaumbele, hivyo wahandisi wachache waliomo nchini ambao wangependa kujiendeleza, fedha zake zipo za kutosha kusomesha wataalamu hao.

Alisema kituo hicho bila kuwa na wataalamu wa kutosha hakitafanya kazi kwa ufanisi unaotarajiwa, hivyo ametaka ufanyike utaratibu ndani ya mwezi mmoja wapatikane watu wa kwenda kufundisha watumishi wengine.

Alitoa wito kwa hospitali hiyo kuendelea kukitunza kituo na vifaa vyake ili kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Wizara tunawataka kituo hiki kiwe kikubwa na uwezo mkubwa kuliko leo na siyo kupunguza malengo yake," alisema.

Meneja wa Mradi wa HPSS Tuimarishe Afya, Ally Kebby, alisema mradi huo umechangia Sh. milioni 300 kwenye uanzishaji wa kituo hicho, fedha zilizotumika katika ujenzi, ununuzi wa vifaa na kompyuta ili kufanya kazi kisasa.

"Kituo hiki ni cha kipekee katika kutoa huduma za ufundi kwenye eneo la afya na kinaweza kuwa cha tatu Kusini mwa Jangwa la Sahara," alisema.

Alisema miaka minane ya awali ya utekelezaji wa mradi huo, walianza kwa kusaidia masuala ya menejimenti na ukarabati wa vifaa tiba kutokana na kutokuwapo na ufanisi kwenye eneo hilo.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Itikadi na Uenezi, Paul Makonda (kushoto), akiteta jambo na Katibu Mkuu wa Chama hicho, Daniel Chongolo alipofika ofisini kwake katika Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya CCM Lumumba, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya kujitambulisha na kuanza kazi rasmi. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# RC Serukamba ahimiza kilimo hai

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amezindua Mradi wa Kijani Hai ambao unalenga kulinda mazingira na kuwataka wakulima kuzingatia kilimo hai.

Amesema mazao yanayozalishwa kupitia kilimo hicho yana mahitaji makubwa katika masoko ya kimataifa.

Akizungumza jana na wakuu wa wilaya, wakurugenzi, maofisa kilimo na wakulima kutoka mikoa ya Singida na Simiyu ambako mradi huo utaendeshwa, Serukamba alisema ni ukweli usiopingika kuwa mazao yanayolimwa kwa kilimo hai yana soko kubwa na yanaweza kuuzwa katika soko lolote duniani.

"Dunia ya sasa lazima uanzie sokoni, ulime kitu ambacho kina mnunuzi, si wakati wa kulima tu, hujui nani atanunua, tulime tukijua mnunuzi ni nani, tukijua mnunuzi ni nani tutalima kulingana na masharti yake," alisema.

Serukamba alisema hivi sasa kuna tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira, hivyo ifike wakati shughuli za uzalishaji ziendane na kuokoa mazingira kwa kuendesha kilimo ambacho hakiharibu ardhi.

"Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza kutunza mazingira kwenye kilimo na vyanzo vya maji, hivyo ninaziagiza halmashauri kuwaelimisha wakulima kutumia kilimo hai ambacho hakiharibu mazingira na pia soko la mazao yanayozalisha kwa njia ya kilimo hicho lipo," alisema.

Alisisitiza suala la matumizi ya mbolea ya asili ili kupata mazao hai na kulinda ardhi iendelee kuwa hai na kwamba mikoa ya Singida na Simiyu itaendelea kutoa ushirikiano katika kilimo hai ili wakulima wajikite kwenye kilimo hicho.

Kiongozi wa Mradi wa Kijani Hai, Andrew Mphuru, alisema mradi huo ambao utaendeshwa kwa miaka mitano kuanzia 2023 hadi 2028, utawanufaisha wakulima 300,000 wa mikoa ya Singida na Simiyu na utagharimu zaidi ya Sh. bilioni nne.

Alisema kuwa kupitia mradi huo ambao utaendeshwa na Shirika la Helvetas kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ) kwa ufadhili wa Laudes Foundation la Uholanzi, wakulima watapewa mafunzo ya namna ya kuendesha kilimo hai cha pamba.

Mphuru alisema lengo la mradi huu ni uzalishaji pamba hai na mazingira ambapo unafanyika kwa sababu wapo wadau wengi wanaotaka kununua pamba hai hasa ikizingatiwa Tanzania ndiyo nchi inayoshika namba moja Afrika kwa uzalishaji wa pamba hai na kuwapo na mahitaji makubwa.

"Kama mnavyokumbuka wiki moja au mbili zilizopita, Rais Samia alifanya ziara katika Mkoa wa Singida, alizungumzia suala la uboreshaji mazingira. Kwahiyo, mradi huu umekuja muda mwafaka," alisema.

Aliongeza kuwa mradi huo unafanyika katika mikoa hiyo kwa kuwa takwimu zinaonesha wakulima wanazingatia kilimo cha pamba hai.

Mkurugenzi wa Mradi wa Kijani Hai kutoka Shirika la GIZ, Hendrick Buermann, alisema wameamua kuja na mradi huo kwa kuwa kwa miaka sita mfululizo wakulima katika mikoa hiyo wanatekeleza kilimo hai kwa kushirikisha zaidi ya wakulima 6,000.

Buermann alisema kupitia kilimo hai wakulima wameweza kunufaika kwa kuongeza uzalishaji na kupata soko la uhakika la mazao yao kwa kuwa hawatumii dawa katika uzalishaji.



# Zanzibar kuimarisha mawasiliano hadi vijijini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA wa Serikali ya Zanzibar, Shukuru Awadh Suleiman, amesema itahakikisha huduma za mawasiliano ya mtandao na miundombinu yake inaimarishwa ili kuwafikia wananchi wote hadi vijijini.

Katika hafla ya utiaji saini makubaliano (MoU) kati ya wakala huo na Kampuni ya Tigo-Zanzitel, Suleiman alisema makubaliano hayo yanalenga kufanya upembuzi yakinifu kuhusu mikakati ya kufikisha huduma hizo vijijini ili kuharakisha maendeleo na biashara.

Alisema hatua hiyo itawezesha wananchi kupata huduma ya mawasiliano kwa kuunganishwa na dunia yote na kufanya shughuli za kibiashara ikiwamo miamala ya fedha.

Suleiman alisema kazi inayotarajiwa kufanywa kwa sasa ni utafiti kuhusu utekelezaji mradi huo na maeneo ya vipaumbele.

"Serikali ya Zanzibar iko katika hatua za mwisho za utekelezaji miradi minne ya mawasiliano ya miundombinu ya TEHAMA ikiwamo ujenzi wa kituo kikubwa cha uhifadhi wa taarifa," alisema.

Alibainisha mradi mwingine unaotarajiwa kutekelezwa ni wa kutenga jumla ya hekta 71 katika maeneo huru ya kiuchumi huko Pemba kwa ajili ya kujenga kijiji cha kidigitali.

"Hiyo ndiyo miradi mikubwa ya kimkakati ambayo tunatarajia kuitekeleza katika kipindi cha mwaka mmoja. Tunataka kuona huduma za mawasiliano ya mtandao yanawafikia wananchi wetu hadi vijijini, hatua ambayo itakuza na kuimarisha utalii," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni Tigo Zantel, Kamal Okba alisema wako tayari kufanya utafiti ambao utasaidia kuleta mageuzi makubwa ya mawasiliano kwa wananchi.

Alisema huduma za mtandao ni muhimu kwa ajili ya mchango mkubwa wa sekta ya utalii katika maeneo ya pembezoni mwa fukwe za Unguja na Pemba.

"Tigo Zantel tupo tayari kutoa mchango wetu mkubwa na kufanya kazi na serikali ya Zanzibar katika kukuza huduma za mawasiliano ya TEHAMA kuona yanawafikia wananchi wote ikiwamo waliopo vijijini katika kukuza utalii," alisema.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefikisha mkongo wa taifa katika wilaya zote 11 za Unguja na Pemba hatua ambayo inatajwa kurahisisha upatikanaji huduma hizo kwa wananchi.




Mkurugenzi wa Wakala wa Miundombinu ya Tehama wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Shukuru Awadhi (kulia), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi wa Tigo – Zantel, Kamal Okba mjini Zanzibar jana, baada ya kutiliana saini makubaliano kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu kuhusu ufikishaji wa huduma za intaneti vijijini. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sensa ya kilimo kuiwezesha serikali kutatua changamoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Seif Shaaban Mwinyi, amesema sensa ya kilimo ni muhimu kwa kuwa itabainisha changamoto zinazoikabili sekta na hivyo kuiwezesha serikali kupanga mikakati ya kuzitatua.

Akifungua mafunzo ya wadadisi wa utafiti wa kilimo wa mwaka 2022-2023 huko Mazizini mjini Unguja, Mwinyi alisema serikali imefanikiwa kuwaletea maendeleo wananchi kwa kutumia takwimu rasmi katika kupanga mipango ya maendeleo.

Pia alisema sensa hiyo inafanyika wakati mwafaka ambao taifa linaelekeza nguvu zake katika kujenga na kuimarisha sekta ya kilimo.

Alisema sekta ya kilimo ni miongoni mwa sekta tano muhimu katika uchumi wa Zanzibar ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza umaskini na kuongeza kipato na uhakika wa chakula.

Alisema sekta ya kilimo inayojumuisha mazao, mifugo na maliasili za misitu ni tegemeo kubwa kwa uchumi wa Zanzibar na inachangia moja kwa moja kwa wananchi katika kujikimu kimaisha.

Mwinyi alisema sekta hiyo imeajiri takribani asilimia 40 ya wananchi wa Zanzibar na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanaitegemea katika kujikimu kimaisha.

Alibainisha kuwa kilimo cha mazao kinachangia asilimia 7.3, mifugo asilimia 12.9, misitu asilimia 1.1 na sekta ya uvuvi asilimia 4.5.

Alisema lengo kuu la mafunzo hayo ni kutoa uelewa wa pamoja kwa wadadisi kuhusu makadirio ya uzalishaji mazao, mifugo na maeneo ya kilimo katika mikoa yote ya Zanzibar.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, alisema ni utafiti huo unahitajika katika kufuatilia na kutathmini malengo yaliyowekwa katika sera na mipango ya maendeleo ya kuendeleza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Alisema utafiti huo utafanyika kisayansi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo itapunguza gharama za kukusanya na kuchakata takwimu hizo kwa kiasi kikubwa.

"Wadadisi hawatatumia tena karatasi, badala yake watatumia kishkwambi chenye dodoso na taarifa zilizokusanywa zitawekwa humo," alisema.

Ali alisema jumla ya maeneo ya kuhesabiwa watu 118 yatapitiwa katika utafiti huo, ambapo wadadisi 25 na wasimamizi watano watafanya kazi huko.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa wadadisi kwa kutoa taarifa sahihi ili serikali ipange mipango ya maendeleo endelevu katika sekta ya kilimo.

Tangu Tanzania ipate uhuru, utafiti na sensa za kilimo na mifugo umeendelea kufanywa. Mara ya mwisho ulifanyika mwaka 2016/17 na kufuatiwa na sensa ya kilimo na mifugo iliyofanyika mwaka 2019/20.

## Mmomonyoko maadili kwa vijana wachangia kusambaa picha 'chafu'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUKOSEKANA malezi bora kumetajwa ni moja ya sababu za mmomonyoko wa maadili kwa vijana unaochangia changamoto ya kusambazwa kwa maudhui ya ngono na utapeli wa mtandaoni.

Mratibu Msaidizi wa Jeshi la Polisi kutoka Kitengo cha TEHAMA, Dk. Dawson Msongaleli, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari visiwani Zanzibar kuhusu Siku ya Usalama wa Mitandaoni.

Alisema pamoja na jitihada wanazozifanya kukabiliana na uhalifu wa kimtandao, mmomonyoko wa maadili ni chanzo cha tatizo hilo.

"Kukosekana malezi bora kwenye familia kumewafanya vijana ambao hawana maadili kuwadhalilisha wanawake na watoto mtandaoni," alisema.

Msongaleli alisema hali hiyo imesababisha kusambaa picha za ngono na katika kufikia usalama wa mtandaoni, lazima jamii irudi kwenye misingi ya malezi bora katika familia.

Mkurugenzi wa Usalama wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Stephen Wangwe, alisema mitandao haina mipaka ya kijiografia, hivyo kila nchi inatakiwa kuwa na sheria za usalama mtandaoni.

Alisema kuwa kwa mujibu wa ripoti ya kukabiliana na masuala ya kimtandao, Tanzania imekuwa nchi ya pili Afrika katika ustahimilivu wa kimtandao.

Alisema Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa tatu; udhalilishaji mtandaoni, utapeli mtandaoni na wizi wa akaunti kwa watu wenye wafuasi wengi katika mitandao.

Mkurugenzi huyo alitoa tahadhari kwa jamii kwa kuitaka kuwa makini katika matumizi ya mtandao kwa kuhakikisha si kila jambo linapaswa kuwekwa mtandaoni.

Mwakilishi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amos Mpili, alisema utafiti uliofanywa kuhusu hali ya ukatili dhidi ya watoto mtandaoni, unaonesha wastani wa watoto 20,000 wenye umri miaka kati 12 na 17 wameshawahi kufanyiwa ukatili mtandaoni.

Alisema utafiti huo umeonesha kuwa asilimia 67 ya watoto wa umri huo, hutumia mitandao ya simu ikiwamo mitandao ya kijamii kama Facebook, Twitter na WhatsApp, ambayo huwaunganisha na watu tofauti duniani. Miongoni mwao, wapo ambao hawana nia njema na kuwalazimisha kutuma picha za ngono.

"Hatutakiwi kuwaacha watoto kuwa na uhuru wa kufanya analolitaka katika mtandao. Tunapaswa kutoa elimu ili kuwa salama anapokuwa mtandaoni," alisema Mpili.

Jumla ya kesi 36 zinazohusiana na makosa ya kimtandao ziko katika mahakama mbalimbali nchini.



**CHINO**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII







# DNA PEKEE INATOSHA

SAUTI zinazidi kupazwa kila upande baada ya mwanamuziki nyota nchini, Diamond Platnumz, kuonekana kumtenga mtoto wake Dylan aliyezaa na Hamisa Mobetto, zikitaka vipimo vya vinasaba (DNA) vifanyike ili kutatua mzozo huo.

Watu kadhaa wametoa maoni yao katika mitandao ya kijamii wakitaka pande mbili husika yaani Diamond  na Hamisa kukubalina kufanya vipimo vya DNA ili ijulikane nani baba halali wa mtoto huyo.

Taarifa kutoka vyazo vya karibu na Hamisa, inaeleza yeye hana kipingamizi na wito unaotolewa wa kufanyiwa vipimo hivyo, ametoa uhuru kwa Diamond kutafuta hospitali yoyote ya ndani na nje ya nchi kufanya kazi hiyo.

Wito huo umezidi kutolewa baada ya tukio la hivi karibuni la Diamond kuambatana na watoto wake watatu pekee katika ziara yake nchini Rwanda, huku mtoto aliyezaa na Hamissa akiwa ameonekana kutengwa katika familia hiyo.

Diamond ana watoto wanne kwa mama tofauti ambao ni Latifa na Nillan aliyezaa na Zari Hassan wa Uganda, Dyllan ambaye mama yake ni Hamissa Mobeto na Naseeb Jr mama yake ni Tanasha Dona kutoka Kenya.

Baadhi ya watu waliitaka serikali kuingilia kati suala hilo kwa kusimamia zoezi hilo ili haki ipatikane kwa kila upande.

Wamesema hatua ya kutengwa waziwazi na baba yake linaweza kuja kumuathiri akiwa na utimamu wa akili, hivyo kuna umuhimu kupata majibu ya mgogoro huo kupitia vipimo vya vinasaba.

Hata hivyo, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dorothy Gwajima ametolea kauli sakata hilo akisema kuna vyombo maalumu vinavyoshughulikia matatizo kama hayo, hivyo utaratibu lazima ufuatwe.

"Unajua huduma za jamii tumesogeza karibu na jamii kama zilivyosogezwa huduma nyingine zote. Hivyo hawa wazazi kama wana mgogoro wowote mahala sahihi sio mtandaoni bali ni kwenye huduma za ustawi wa jamii, halimashauri au mkoa au kituo chote cha polisi karibu nao. Dawati la jinsia lakini pia tuna namba 116 ya dharura zote kuhusu masuala ya watoto na jamii," amesema Waziri Gwajima.

BASI SAWA

## Chino ataka wamuelewe



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Chino amesema watu wasimkariri mtu kwani inafikia wakati anabadilika kutokana na nyakati.

Amesema wimbo wake alioimba na Stamina ameonyesha jinsi alivyobadili mwelekeo wake wa kimuziki kutoka Amapiano ambao wengi wameuzoea hadi ngoma ya Hiphop.

"Kuna watu wengi wataweza kupata majibu ya mimi kubadili muziki kutoka amapiano hadi hip hop. Kitu ninachojivunia wapo wanaoelewa kwamba nipo kila kona ila kutokana na mafanikio naweza kutengeneza matatizo mengine," amesema.

## Rotimi kampoza Vanessa kiaina



MWANAMUZIKI na mcheza filamu wa Marekani, Rotimi ambaye ni mume wa Vanessa Mdee, ametambulisha singo yake mpya inayoitwa Bestie yenye mahadhi ya kimahaba.

Ngoma hiyo iliyoachiwa siku tatu zilizopita inafanya vizuri kwenye majukwaa mbalimbali ya muziki duniani.

Rotimi na Vanessa wamekuwa katika maisha ya pamoja kwa zaidi ya miaka minne na ujio wake huo unawaweka katika hali ya mkao wa utayari mashabiki wake kupokea kazi yake nyingine inayoitwa Even.



# PHINA, FAHYVANN KULIKONI TENA?

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Saraphina maarufu kama Phina yupo kwenye bifu zito na mpenzi wa Rayvanny, Fahyvanny baada ya hivi karibuni kutofautiana kimtazamo kuhusu dhana ya wanawake weupe wanavyopendwa na wanaume.

Phina aliingilia kati baada ya Fahyvanny kutoa maoni yake kwamba wanaume wengi hata ndani ya nafsi zao wakiulizwa kuchora taswira ya wanawake wanaowawazia kuwaoa au kutoka nao kimapenzi basi watataja wenye ngozi nyeupe.

Kulingana na Phina, alipinga dhana hiyo na kueleza ngozi nyeupe haina thamani yoyote kwani siku hizi warembo wengi huinunua katika maduka ya vipodozi lakini ngozi nyeusi huwezi kuipata popote.





## Harmonize ajibembeleza kwa Hamissa

MWANAMUZIKI mkali wa Bongo Fleva, anazidi kuimarisha zoezi lake la kumfukuzia kimapenzi mwanamitindo Hamissa Mobeto, kiasi ambacho sasa ameonekana kama amepagawa.

Katika kile kinachoonekana Harmonize kapagawa kiasi ambacho hasikii wala haoni ni pale alipoamua kuweka picha ya kuchorwa akiwa yeye na Hamisa katika pozi la kama mume na mke.

Mchoraji huyo aliwachora Hamisa na Harmomize wakiwa kwenye mwonekano wa kimahaba jambo ambalo lilimfanya mwanamuziki huyo kuiweka picha hiyo kwenye ukurasa wake wa Instagram kama ishara ya ndoto njema kwake.

# MASTAA HAWA WALIKUFA KWA AJALI

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA ni moja kati ya nchi zilizojaliwa kupata wasanii na wanamuziki wakubwa, mahiri na tishio kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Si kwenye muziki wa dansi, taarabu, bongo fleva, na hata waigizaji, Tanzania imebahatika kupata wanamuziki ambao wameipatia heshima kubwa nchi hii kwenye masuala la muziki.

Hata hivyo kwa bahati mbaya wengi wao wamefariki kwa sababu mbalimbali, ikiwemo maradhi na ajali.

Rekodi zinaonyesha kuwa baadhi ya wanamuziki wakubwa Tanzania wamefariki kutokana na ajali za barabarani na kuacha vilio, huzuni na simanzi kwa mashabiki wa muziki.

Leo tutawaangalia wanamuziki na wasanii bora kabisa nchini, ambao walifariki dunia kutokana na ajali za barabarani.

**Salum Abdallah**

Ni mmoja wa waasisi wa muziki wa Tanzania. Salum Abdallah alizaliwa mwaka 1928 mjini Morogoro kwa baba Mwarabu raia wa Yemen na mama mwenyeji wa mkoa wa Morogoro.

Hadi leo hii, licha ya kwamba alifariki mwaka 1965, lakini baadhi ya nyimbo zake ni maarufu hadi leo. Nyimbo hizi ni 'Mkono wa Idd', 'Shemeji Shemeji huku Mwazima Taa, ' Wanawake Tanzania', 'Ngoma Iko Huku', 'Nina Mpenzi wangu Kibambaye' na nyingine nyingi.

Alifariki mwaka 1965 kwa ajali ya gari, baada ya lori lake la mchanga alilokuwa akiendesha kugonga ukingo wa daraja na kumtupa nje. Ajali hiyo ilitokea mkoani Morogoro wakati alipotoka kulikwamua lori hilo lililokuwa limekwama na kulirudisha nyumbani.

**Mbaraka Mwinshehe**

Huyu pia ni mwanamuziki aliyetokea Morogoro kama Salum Abdallah. Ni mwanafunzi wa Salum pia. Alizaliwa Morogoro mwaka 1944 na kutokea kuwa mwanamuziki mkubwa mno Afrika Mashariki na Kati.

Alikuwa mwimbaji na mpiga gitaa kwenye bendi ya Moro Jazz, na ilipofika mwaka 1973, aliunda kundi lake la Super Volcano. Moja ya wimbo wake bora ambao hadi leo unapendwa na vizazi kwa vya sasa ni 'Shida'.

Alifariki Januari 12, 1979 Mombasa nchini Kenya alipokuwa amekwenda kwenye kazi zake za muziki.

Gari dogo la rafiki yake alilokuwa amepanda liligonga lori lililokuwa limeegeshwa na kufariki dunia.

**Abuu Semhando 'Baba Diana'**

Ni mwanamuziki mkongwe, mpiga drums wa bendi za Tanga International, Super Matimila, Tomatoma, Vijana Jazz na mwishowe African Stars 'Twanga Pepeta'.

Alifariki dunia usiku wa kuamkia Desemba 18, 2010, baada ya pikipiki alilokuwa akiendesha kutoka kwenye onyesho la Twanga Pepeta, kugongwa na gari eneo la Mbezi Beach, Dar es Salaam na kusababisha kifo chake.

**Issa Kijoti**

Mwimbaji wa muziki wa taarabu aliyekuwa akichipukia, baada ya kutoa wimbo wake wa 'Usinijadili' ambao ulikuwa na kionjo kilichoondokea kuwa maarufu kilichoimbwa hata na watoto mitaani 'nichumu, nichumu tena, mwaaa', Issa Kijoti, alifariki dunia 2011, baada ya basi dogo walilokuwa wakisafiria kutoka Mbeya walikokwenda kimuziki, kugonga lori lililokuwa na mbao, ambalo basi hilo lilitaka kulipita mkoani Morogoro.

Kijoti, aliyekuwa kiongozi wa Five Star na maarufu wakati huo, alifariki dunia na baadhi ya wanamuziki wenzake.

**Sharo Milionea**

Ndiyo alikuwa ameshaanza kuwa maarufu na kuanza kupata mafanikio ya kazi yake ya uigizaji wa ucheshi.

Sharo Milionea, jina halisi Hussein Ramadhani, wakati anaanza kuonja mafanikio, baada ya msoto wa kufika hapo, alipata ajali mwaka 2012 katikati ya maeneo ya Segera na Muheza. Akiwa anakwenda kwao mkoani Tanga, gari alilokuwa akiendesha aina ya 'Toyota Harrier' alipokuwa akitoka kwenda Muheza, lilipinduka baada ya kuacha njia kwenye eneo linaloitwa 'Maguzonizonga', na kusababisha kifo chake.

FILAMU

## Talaka Tatu: Mke wa mtu sumu

**Na Adam Fungamwango**

LEO tunaiangalia filamu iitwayo 'Talaka Tatu', ambayo imechezwa na wasanii Salim Ally, Ibrahim Matutu, Chiku Mashemashe, Amina Rashid, Salha Niwako, Rehema Amir, Isakwisa Sanke, Semeni Kolongo, Anna Msigala na wengineo.

Matutu na mkewe Zuhura wanaishi raha mustarehe. Lakini kuna kijana mmoja mtaani anaitwa Makame, yeye hali halali kwa Zuhura.

Anatokea kumpenda mwanamke huyo kiasi cha kuwatuma mpaka dada zake. Lakini wakakataa kwa sababu wanafahamu kuwa Zuhura ameolewa.

Makame anaamua kumvaa mwenyewe na kumuelezea hisia zake, lakini anakataa akimwambia kuwa yeye ni mke wa mtu hawezi kufanya kitu kama hicho.

Matutu anapata safari ya kikazi ambayo anakwenda kukaa miezi mitatu. Safari hiyo ilikuwa ni kama msiba kwake. Makame akazidi kukaza uzi na hatimaye upweke uliomkumba Zuhura anaamua kumkubalia.

Mumewe anarejea kabla ya miezi hiyo bila kumwambia mkewe, anampigia simu mkewe anamwambia yupo nyumbani wakati Matutu alishafika kitambo.

Aliporudi akaona hata haya. Mabadiliko ya mkewe yalianza kumtia wasiwasi Matutu. Akachukua simu ya mkewe na kukuta meseji za mapenzi.

Kuna siku anadanganya mama yake mzazi anaumwa ili aende kwa mpenzi wake Makame, lakini alipoondoka mama yake Zuhura alikuja kumtembelea binti yake na hakumkuta.

Matutu hakutaka mama ajue chochote, akamdanganya kuwa amekwenda kwa rafiki yake.

Siku si nyingi akapata matatizo ya macho na kuwa kipofu. Hii ilileta huzuni kubwa. Kwa mkewe ilikuwa poa tu kwani alikuwa sasa akimwingiza Makame humo humo ndani.

Siku ya siku akakuta wanakula pamoja. Akaanza kuwazodoa na kuwasuta. Ndipo alipowaambia yeye si kipofu alikuwa akijifanya tu ili aangalie yaliyokuwa yakiendelea. Akampa mkewe talaka tatu hapo hapo.

Makame na Zuhura kwa aibu wakaondoka na kwenda kuishi pamoja. Siku si nyingi Zuhura akakuta Makame si mwaminifu na alipomuuliza alitukanwa na kutimuliwa.



BT BURUDANI TELE



# Kcee kuburudi sha AMAA 2023

WAANDAAJI wa Tuzo za Africa Movie Academy Awards (AMAA) wametangaza mastaa wanne wa muziki watakaoburudisha katika kilele cha utoaji tuzo Oktoba 29 jijini Lagos.

Mkuu wa Kiufundi wa AMAA 2023, Kingsley James amefichua kwamba wanamuziki maarufu Kingsley Okonkwo, maarufu Kcee, Yinka Davies (Camido) na Zadok Aghalengbe ambaye ni mshiriki katika toleo la saba la Nigerian Idol, watatumbuiza katika tuzo hiyo ya filamu.

Tuzo hiyo itafanyika katika ukumbi wa Balmoral Convention Centre, Sheraton Hotel jijini Lagos.



## DJ Cuppy apata dili zito

MNIGERIA Florence Otedola, maarufu kama DJ Cuppy, amepata dili la kuandaa muziki wa Afribeats ambao utatumika kuwaburudisha wasafiri watakaotumia shirika la ndege la British Airways.

Ofisa mkuu wa wateja wa shirika hilo, Calum Laming, amesema orodha hiyo itaanza kutumika Novemba mosi mwaka huu.

Amesema DJ Cuppy, ambaye ujuzi wake ulimpeleka katika zaidi ya nchi 30 duniani kote, ameanza kuratibu nyimbo katika mfumo wa burudani ndani ya ndege ya shirika hilo.

## Burna Boy sawa na moto

BAADA ya kupata mafanikio katika muziki tangu 2018, msanii maarufu wa muziki wa Afrobeats kutoka Nigeria, Burna Boy amepanda hadhi ya nyota na muziki wake kumshindia tuzo nyingi na kuuza kumbi bora ulimwenguni.

Katika tukio lingine la kihistoria, Burna Boy anakuwa msanii wa kwanza wa Kiafrika kuwa na albamu tano ambazo zimepata watu milioni 200 kwenye mtandao wa ununuzi wa muziki wa Spotify.

Burna Boy alipata mafanikio ya kimataifa kwa wimbo wake wa 'YE' mwaka 2018 na kufuatia albamu yake iliyosifika kibiashara 'African Giant' ambayo ilimpatia uteuzi wake wa kwanza wa tuzo za Grammy.





## Hailey wanakutakia mema

MKE wa mwanamuziki wa Pop, Justin Bieber anayeitwa Hailey Beiber amesema amechoshwa na uvumi unaoendelea kuwa ana ujauzito.

Akizungumza katika mahojiano ya hivi majuzi, amesema uvumi huo unaoibuka mara kwa mara umemuathiri kiakili.

Amesema amechoshwa na kukanusha madai hayo kila wakati na kufafanua tumbo lake lina kawaida ya kuvimba , lakini hakuna kiumbe ndani.

## Paris huo ndo uzazi

MWANAMITINDO tajiri wa Marekani,Paris Hilton amekasirishwa na baadhi ya wafuasi wake wanaomsema vibaya mtoto wake wa miezi minane Phionex.

Watu wameibua mjadala mitandaoni baada ya picha alizoziweka Paris akionekana akiwa na mtoto wake huyo ambaye ana mwonekano wa kichwa kikubwa.

Amesema maoni ya watu kuhusu kichwa cha mwanawe yamemuumiza na ni sawa na unyanyasaji na kusisitiza Phionex yuko sawa na ukubwa wa kichwa chake unatokana na ubongo kuwa mkubwa.





## Tanzania kushiriki mkutano mabadiliko tabianchi Dubai

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TANZANIA imeanza maandalizi kwa ajili ya kushiriki mkutano wa 28 wa mkataba wa mabadiliko ya tabianchi unaotarajia kufanyika Dubai.

Mkutano huo unatarajia kufanyika kuanzia Novemba 30 hadi Desemba 12 mwaka huu kwa siku mbili. Utatoa nafasi kwa wakuu wa nchi zote duniani kutoa matamko mbalimbali kuhusu juhudi walizozifanya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Kaimu Mkurugenzi anayeshughulikia Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Paul Degratius, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati wa kikao cha ufunguzi wa maandalizi kilichowakutanisha wataalamu kutoka ofisi hiyo na wadau.

Alisema katika mkutano huo, Tanzania itakuwa na banda maalum ambalo watalitumia kuonesha vitu mbalimbali ambavyo vinafanyika ikiwamo shughuli za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema wakati wakijipanga kuelekea katika mkutano huo, msimamo wa nchi umelenga kuongeza kasi ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Sisi kama Tanzania tunapokwenda kule ni lazima tufahamu tunakwenda kufanya nini? Ndio sababu tumeandaa msimamo wa nchi kwa kuwa, tunataka kila mmoja atakapokwenda tuzungumze kitu kimoja ili tutakaporejea tuwe tumepata kitu chenye manufaa kwa taifa letu,"alisema.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, alisema Tanzania inakwenda na kaulimbiu ambayo imejikita zaidi kwenye masuala ya kilimo, uchumi wa buluu na nishati safi.

"Kwa upande wa sera, tunatakiwa zaidi kuandaa miongozo na kanuni ambazo zitaisaidia nchi kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Sisi kama nchi tumeshaandaa sera ambayo tuliizindua mwaka 2001, na tunatekeleza namna ya kukabiliana na athari hizo. Pia tumeandaa sera ambayo nchi inachangia namna ya kupunguza uzalishaji wa gesi joto duniani ambapo tumeweka malengo yetu na tunatekeleza kila mwaka," alisema.

Mwakilishi wa Benki ya Dunia (WB), Innocent Esikuri, alisema wamekuwa ikitoa mchango kwa kutoa msaada kwenye masuala ya mazingira kwa nchi za Afrika ikiwamo Tanzania.

Pia alisema wamekuwa wakiyajengea uwezo makundi mbalimbali kwa ajili kukabiliana na mabadiliko ya tabiachi.

Alisema Tanzania ni nchi ya tatu katika Bara la Afrika kwa kuwa na misitu mingi na mikubwa, hivyo wako tayari kusaidia sekta hiyo, kwa lengo la kuhifadhi na kutunza mazingira.

Mwakilishi wa Ubalozi wa Uingereza nchini, Abdala Mwikama, alisema nchi hizo zimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu kwenye mambo mbalimbali ikiwamo la mabadiliko ya tabianchi.

"Uingereza imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya kusaidia utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na athari zinazojitokeza duniani,"alisema.

# Haja ndogo yenye harufu kali dalili kutonyonyeshwa vizuri

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

OFISA Lishe wa Mkoa wa Manyar, January Dalushi, amesema mtoto kushindwa kuongezeka uzito, kutoa haja ndogo kidogo au yenye harufu kali ni viashiria vya mtoto kuwa hanyonyi vizuri.

Amesema hali hiyo huathiri ukuaji wa mtoto kama wazazi na walezi hawatachukua hatua za haraka.

Dalushi alibainisha hayo jana katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi kuhusu maziwa ya mama yanavyochangia ukuaji wa mtoto kuanzia miaka sifuri mpaka miaka mitano.

Alisema ili kujua mtoto ananyonya vizuri, akipelekwa kliniki wanaangalia angalau awe ameongezeka uzito gramu 500.

"Na ukitaka kujua mtoto ananyonya vizuri maziwa ya mama, anakuwa anatoa haja ndogo mara kwa mara, ila mkojo kama ina harufu kali sana, huyo hanyonyeshwi sana," alisema Dalushi.

Alisema mtoto anatakiwa kunyonyeshwa mara kwa mara kadri anavyohitaji. Viashiria vya watoto kuwa na njaa ni kulamba midomo, kunyonya kidole au vidole au kulia.

Alikumbusha kuwa maziwa ya mama ni chakula pekee na kinywaji cha mtoto wa mwenye umri kuanzia sifuri mpaka miezi sita na ndiyo hujenga ubongo wake.

"Asilimia 80 ya maziwa ya mama yana maji ndiyo maana huwa tunashauri mtoto asipewe maji maana yamo kwenye maziwa ya mama," alisema.

Dalushi alisema maziwa ya mwanzo yana faida kubwa hasa yale ya njano ya ndani ya siku mbili ambayo mtoto hatakiwi kuyakosa.

"Wanaokamua maziwa ya mama ili kumhifadhia mtoto hayahitaji jokofu bali hutakiwa kuhifadhiwa kwenye chombo cha kawaida kisafi kwa saa sita mpaka nane na mtoto asipewe kwa chuchu, apewe kwa kikombe cha kawaida," alieleza.

Mtaalamu huyo alisema ni lazima maziwa yawe kwenye joto la nyuzi joto 35 mpaka 36 ambalo ni joto la kawaida la binadamu. Alibainisha kuwa maziwa yakihifadhiwa kwenye jokofu yanaweza kutunzwa mwaka mzima.

Alisema mama anapojifungua anatakiwa kuongeza idadi ya milo kwa kula kati ya mitano mpaka sita na kati yake, minne iwe mikubwa na miwili iwe midogo midogo ambayo inaongeza virutubisho kwenye mwili wa mama.

Dalushi alisema mtoto anaponyonyeshwa vizuri, anaepuka kupata ugonjwa wa manjano, anaimarika kinga za mwili, kupunguza maambukizi ya kuhara, kisukari, saratani, vifo vya watoto na kuimarisha ukuaji wa akili na misuli.

Mshauri wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC), Davis Gisuka, alisema ili ubongo uweze kufanya kazi vizuri, ni lazima mtoto apate chakula bora.

Gisuka alisema matendo ya wazazi yanasaidia mtoto kukua na kusisitiza kuwa mama anaponyonyesha anapaswa kumwangalia usoni mtoto wake au kumwimbia.

Mzazi Veronica Mushi alisema baada ya kufanyiwa operesheni, aliletewa mtoto wake na kumnyonyesha ndani ya saa moja.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, asilimia 97 ya watoto wanaozaliwa hunyonyeshwa maziwa ya mama na asilimia 43, hunyonyeshwa miaka miwili na kuendelea huku asilimia 90 hunyonyeshwa ndani ya saa moja nchini.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Umoja wa Wakulima na Uhifadhi wa Mazingira (UWAMAKIZI), wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Twaha Mbarouk (kushoto), akikabidhi mahindi kilo 200 kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari ya Potwe, Mulla Suleiman (kulia), kwa ajili ya chakula kwa walimu na wanafunzi wa shule hiyo mapema wiki hii. Katikati ni Diwani wa Viti Maalum, Fikira Madege. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanaoanza pombe chini ya miaka 15 hatarini zaidi

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

UTAFITI unaonesha vijana wanaoanza kunywa pombe kabla ya umri wa miaka 15, wako mara sita zaidi katika hatari ya kuwa na matatizo ya utegemezi wake kuliko wale wanaoanza kunywa baada ya umri wa miaka 21.

Meneja wa Mawasiliano na Uendelevu wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Rispa Hatibu, amesema utafiti uliofanywa na Wizara ya Afya mwaka 2008 (wakati huo ikiitwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii) kwa wanafunzi wa shule za sekondari Mkoa wa Dar es Salaam, ulionesha asilimia tano waligundulika kutumia pombe.

Alisema utafiti huo ulionesha asilimia 10.8 waliitumia kabla ya kufikisha umri wa miaka 14 na asilimia 26.2 walikuwa na mzazi aliyekuwa anatumia pombe.

"Matumizi ya pombe wakati wa utoto na ujana yanaweza kuwa na athari mbaya za kiafya, kijamii, kiuchumi, na kimaendeleo kwa vijana na jamii," alisema.

Kutokana na hilo, alisema kampuni yao imetangaza mwendelezo wa programu yake ya Smashed katika Mkoa wa Tanga ambayo ilianza mwaka 2021 na tayari imezifikia shule 22, ikiwaelimisha wanafunzi 24,025 nchini.

Hatibu alisema lengo la programu hiyo ni kutoa elimu kupitia maonyesho kwa kulenga kuvunja utamaduni wa kunywa pombe kwa vijana wenye umri mdogo na kupunguza madhara yanayohusiana na pombe kwa kundi hilo.

Alisema programu ya Smashed inawakilisha hatua muhimu kuelekea kukuza uchaguzi wenye dhamira na kuwawezesha vijana wa Tanzania kuwa na maarifa na stadi wanazohitaji kufanya uamuzi sahihi kuhusu matumizi ya pombe na kuzuia kabisa matumizi yake kwa vijana walio chini ya umri wa kisheria.

Alisema programu hiyo haihusishi tu uzuiaji wa kutumia pombe kwa vijana, bali pia kuwezesha akili za vijana kufanya uamuzi yenye msingi na dhamira sahihi na kuwatia moyo wanafunzi kutilia mkazo elimu na kuendeleza stadi muhimu, kama vile kutawala hisia zao, ambayo itakuwa zana muhimu katika kushughulikia changamoto za maisha.

"SBL inaelewa kuwa shinikizo la rika haswa vijana ni sababu ya kunywa pombe kwa vijana na ni muhimu kukumbuka kuwa, una uwezo wa kusema hapana na kufanya maamuzi yanayolingana na thamani ya malengo yako.

"Marafiki wa kweli wataheshimu uamuzi wako na kusaidia safari yako. Kama wanafunzi, wote ni sehemu ya jamii kubwa zaidi nje ya shule hizi, na sote tunashiriki jukumu la kujali ustawi wa wenzetu na jamii kwa ujumla.

"Watie moyo marafiki na wenzako kufanya uamuzi sahihi na kupinga kunywa pombe kwa vijana walio chini ya umri wa kisheria," alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Mwanamke wa zamani, piga ua hakosi vifaa hivi nyumbani...

**Na Adam Fungamwango**



Dodoki



Ungo



Mbuzi



Kinu

NIKIKUMBUKA zama zile, mwanamke alikuwa mwanamke na mama ni mama hasa!

Kila ulichotarajia kwa wa jinsia hiyo amekamilika, hata zile stadi za kuhudumia nyumba na kujihudumia mwenyewe, kimama amekamilika.

Aliko mwanamke, iwe amevaa kiofisa au kinyumbani nyumbani, iwe kwa kujificha kwenye pochi zake, au ameamua kuzivaa, piga ua hakosi khanga.

Nenda nyumbani kwake sasa, nyenzo zote za upishi anazo, tena kiwanda kimoja na zile alizotumia kwa mama yake, tofauti labda aina za hapa na pale.

Utamu zaidi sasa, hata vifaa hivyo vimetengenezwa na viwanda vya SIDO au ukoo wake, kwa hapa Dar es Salaam, moja kwa moja ni vile vya Gerezani, kuanzia kibatari, sufuria zile zile ulizopikiwa na mama yako kijijini..., we acha tu!

Enzi hizo unapokwenda nyumbani kwa mtu yeyote ambaye ana mke, au hata mwanamke tu anayeishi naye kuna vitu ambavyo unavikuta na kukuthibitishia kuwa nyumba hiyo ina mtoto wa kike anayeimiliki.

Kwanza kabisa lazima ukute kuna kibao cha mbuzi, hasa kwa akinamama wa mikoa ya Pwani.

Kina mama waliokulia au kuzaliwa kwenye mikoa ya Pwani na hata wakati mwingine kuhamia, walihakikisha nyumbani hakukosi kibao cha mbuzi.

Kazi yake ilikuwa ni kukuna nazi kwa ajili ya kuunga mboga zinazohitaji kuungwa kwa kiungo hicho, futari au chakula kingine kinachohitaji nazi.

Ni tofauti na sasa. Zama zinabadilika. Unaweza kwenda nyumba ambayo anaishi mtoto wa kike usikute kibao cha mbuzi.

Siku hizi bwana, wake zetu, dada zetu wanaenda sokoni, wananunua nazi na kukuniwa huko huko.

Kama si hivyo basi nyumbani kuna mashine ya kukunia nazi, inaitwa kwa kizungu 'coconut scraper', na pia dukani siku hizi wanauza pakti za tui la nazi.

Kila kitu kimeshafanywa kiwandani, unanunua wakati wa kupika chakula kama kisamvu, samaki au maharage, unachofanya ni kuchana pakti na kumimina tui kwenye mboga ikiwa inachemka jikoni.

Kwa maana hiyo wanawake wengi wa sasa wala hawana haja ya kukaa na kibao cha mbuzi ndani.

Wamebaki wachache sana, na hata biashara hiyo inayotembezwa na watu njiani si kubwa sana kama zamani.

Kingine ambacho mwanamke wa zamani unakikuta nyumbani kwake ni kinu cha kutwangia. Achana na kinu kidogo cha kutwangia viungo cha mboga na pilau, hapa nasemea kinu cha kutwangia mahindi, mpunga, na kisamvu.

Kifaa hiki kilikuwa muhimu kwa sababu wakati huo kulikuwa na tabu ya unga na mchele, hivyo mara nyingi kina mama walinunua mahindi na kuyatwanga.

**Kwa sasa si lazima tena. Mwanamke anakwenda sokoni kununua kisamvu anarudi tayari kimeshatwangwa. Kuna watu huko huko sokoni wana kazi hiyo ya kutwanga kwa malipo.**



Jiwe la kusugulia miguu

Halafu pia kwa nyakati hizo ilikuwa ni ufahari kwa mwanamke kuwa na vitu kama hivyo kwa sababu anaonekana amekamilika na anaijali familia yake.

Kwa sasa si lazima tena. Mwanamke anakwenda sokoni kununua kisamvu anarudi tayari kimeshatwangwa. Kuna watu huko huko sokoni wana kazi hiyo ya kutwanga kwa malipo.

Kuna mchele wa kila aina madukani, wala haimlazimu mama wa sasa kununua mpunga na kuanza kuutwanga kwa kinu na mchi.

Kama ataletewa na ndugu zake mpunga kutoka kijijini, atapeleka mashine, kwa maana hiyo wala hawalazimiki kuwa na kinu.

Vingine ni ungo kwa ajili ya kupetea mchele, choroko na nafaka zingine. Baadhi naona hadi leo wanavyo lakini si lazima sana. Hata kama hana maisha yataendelea tu.

Jiwe la kusagia, la kusugulia mguu na dodoki, ni moja kati ya vitu ambavyo huwezi kuvikosa kwa mwanamke wa zamani.

Siku hizi vyote hivyo vimebaki historia. Na tatizo kubwa ni mazingira ya kimaisha yanakwenda yanabadilika.

Na kila tunavyozidi kuendelea mbele, kukua kwa teknolojia tunashuhudia mengi ambayo yatatushangaza.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Wasiwasi watanda baada ya Misri kushambuliwa mabomu ya Israel

**CAIRO,** MISRI

MIJI miwili iliyoko Bahari ya Shamu upande wa Misri jana asubuhi ilishambuliwa kwa makombora na kusababisha watu kadhaa kujeruhiwa.

Tukio hilo limezidisha wasiwasi kusambaa nje ya mipaka kwa mzozo kati ya Israel na Hamas.

Vyanzo viwili vya usalama kutoka Misri vimeliambia shirika la habari la Reuters kuwa milipuko hiyo iliupiga mji wa Taba kwenye mpaka na Israel na wa Nuweiba.

Hakuna yeyote aliyedai kuhusika na mashambulizi hayo, lakini shirika la habari la Al-Qahera lilisema kombora lililoanguka Taba lilionekana kuhusishwa na mapigano kati ya wanamgambo wa Hamas na jeshi la Israel.

Wizara ya Afya ya Misri ilisema watu sita walijeruhiwa katika mji wa Taba. Miji ya Taba na Nuweiba, ambayo inapatikana katika rasi ya Sinai nchini Misri, ni maarufu kwa watalii.

Katika hatua nyingine, vikosi vya Israel vikisaidiwa na ndege za kivita na droni vimefanya shambulizi la pili la ardhini katika Ukanda wa Gaza na kuyapiga maeneo ya viunga vya mji huo.

Hayo ni kwa mujibu wa jeshi la Israel wakati likijiandaa kufanya uvamizi kamili wa ardhini katika eneo hilo linalotawaliwa na vuguvugu la Hamas.

Idadi ya Wapalestina imefika 7,000 wakati Israel ikiendeleza wimbi la mashambulizi makali ya angani kujibu uvamizi uliofanywa na Hamas kusini mwa Israel Oktoba 7.

Idadi hiyo inajumuisha zaidi ya watoto 2,900 na wanawake 1,500.

Wasiwasi umetanda kuhusu hatima ya Wapalestina milioni 2.4 walionasa katika mapigano hayo,

Viongozi wa Umoja wa Ulaya wametoa wito wa kupelekwa msaada wa dharura bila vizuizi kupitia mbinu zozote zile ikiwemo kutengwa kwa maeneo salama ya kiutu na kusitishwa mapigano kwa muda.

Umoja wa Mataifa ulisema jana kuwa msaada usio na kikomo unahitajika Gaza ikiwa ni baada ya wiki tatu za mashambulizi ya Israel.

Kamishna mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA), Philippe Lazzarini, alisema msaada unahitajika Ukanda wa Gaza, akieleza unaoingia sasa ni mdogo kama makombo.

Lazzarini pia amethibitisha kuwa wafanyakazi 57 wa shirika hilo wameuawa katika vita hivyo.

Wakati huo huo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Russia imethibitisha kuwa wajumbe wa Hamas waliwasili nchini humo kwa ajili ya mazungumzo.

Tangazo hilo lilisema ujumbe huo ni wahusika wakuu wa kundi hilo na wanahitaji kutatua mgogoro huo haraka iwezekanavyo.

Hamas haichukuliwi kama kundi la kigaidi kwa Russia, tofauti na nchi nyingine kadhaa ikiwamo Uingereza na Marekani.

Shirika la Habari la RIA Novosti lilisema ujumbe huo uliongozwa na kiongozi mkuu wa Hamas Moussa Abu Marzouk, ambaye anadhaniwa kuishi Doha, nchini Qatar.

Picha iliyowekwa kwenye mitandao ya kijamii ilimuonyesha akikutana na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Mikhail Bogdanov.

Lakini Israel ilisema mikono ya viongozi wakuu wa Hamas imefunikwa na damu ya Waisraeli 1,400 na kuitaka Russia kuwatimua wajumbe hao.

Wizara ya mambo ya nje ya Russia pia imefichua kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran pia yuko katika mji mkuu wa Moscow.

**DW**



Kundi la wanawake na watoto raia wa Sudan wakiwa wamekusanyika kwenye kambi ya wakimbizi baada ya kukimbia mapigano yanayoendelea kati ya kikosi cha kijeshi cha Rapid Support Forces (RSF) na jeshi la serikali. **PICHA: AFP**

## Waziri mkuu China afariki dunia

**BEIJING,** CHINA

WAZIRI mkuu wa zamani wa China Li Keqiang (68) amefariki dunia baada ya kupata matatizo ya mshtuko wa moyo.

Kiongozi huyo alitajwa kuwa kiongozi wa baadaye wa nchi hiyo, kitendo ambacho kilimfanya Rais wa China, Xi Jinping kumweka kando na kumtenga kisiasa.

Vyombo vya habari vya serikali vilisema Li alikuwa amepumzika milele wakati alipokuwa mji wa ko Shanghai alipopatwa na mshtuko wa moyo wa ghafla siku ya Alhamisi.

Aliaga dunia usiku wa manane siku ya Ijumaa licha ya juhudi kubwa za kumpatia matibabu, shirika la utangazaji la serikali CCTV lilisema.

Katika muhula wake wa mwisho akiwa waziri mkuu, uliomalizika mapema mwaka huu, Li alikua ofisa mkuu pekee aliyeko madarakani ambaye hakuwa wa kundi la watiifu la Rais Xi.

Li, mtu wa pili mwenye nguvu katika Chama tawala cha Kikomunisti cha China hadi alipostaafu mwaka jana, alijulikana kama mmoja wa watu werevu zaidi wa kisiasa wa kizazi chake. **BBC**



## Mapigano makali yaitikisa Goma

**GOMA,** DRC

MAPIGANO makali yanaendelea karibu na mji mkuu wa mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, yakihusisha majeshi ya serikali na waasi wa kundi la M23.

Milio ya risasi ilisikika katika eneo hilo baada ya kundi la M23 kupambana na muungano wa vijana wazalendo wanaoungwa mkono na jeshi la DRC.

Vyanzo vya kiraia katika eneo hilo vilisema mapambano ya silaha nzito yamefanywa na jeshi la la serikali dhidi ya ngome za HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/congo-yataka-vikosivya-afrika-mashariki-viondokedrc/a-67051984"M23.

Duru za kijeshi zilisema kuwa lengo ilikuwa ni kuwazuia waasi wa M23 kujipenyeza katika mji wa Goma wakipitia katika mbuga ya wanyama ya Virunga.

Kwa siku mbili milio ya risasi inarindima katika kijiji cha Bambo wilayani Rutshuru ambako waasi wa M23 wanakabiliana na muungano huo wa vijana wazalendo.

Mashambulizi hayo ya kila upande yamesababisha raia kuyakimbia makazi yao na kwenda kuomba hifadhi katika kambi za wakimbizi.

Mkazi mmoja Tyisabe Climantine ambae alitengana na mumewe wakati wa makabiliano ya wanajeshi wa Congo na waasi wa M23, aliambia DW kuwa usalama wa raia eneo hilo ni mdogo. **DW**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



VIVIAN HENRY MAPUNDA anatangaza kupotea kwa Result Slip ya kidato cha sita yenye index namba S.2325/0642 iliyotolewa na CANOSA SEKONDARI mwaka 2023. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: PHQ/DAR/ILA/28499/2023.

## KUPOTEA KWA CHETI



**VICTORIA PHILEMON MARANDU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1075-0033 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia DARAJANI SEKONDARI mwaka 2003. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIN/31529/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEORGE ALEXANDER,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato kuhitimu kidato cha nne chenye index No. S0984-0012 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BUKAMA SECONDARY SCHOOL Mwaka 2003, Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**TAARIFA YA POLISI: MWA/NY/RB/133962/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOHN AMANI MUSHI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T262CLC** aina ya Toyota Grand Hice. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi:

**DOD/DOD/RB/54950/2023**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF RUNGWE DISTRICT**
**AT KIKUYU**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 06 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MOSES MWAKIJULE MWAKIBASA**
**AND**
**FAUSTINA KOKUTONA RUTAKYAMIRWA............APPLICANT**
**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate ( or letter of administration) is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 30th day of NOVEMBER 2023.

Dated at Rungwe this 26th day of OCTOBER, 2023.

DISTIRCT RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
RUNGWE - TUKUYU

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAUDI JOSEPH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba: S.0108.0623, kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia IFUNDA TECH SCHOOL mwaka 2009. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/31579/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWAMJA

Ndugu STANFORD TUMAINI NDALUHEZA amepotelewa na hati ya kiwanja yenye majina ya YOSIA KARIJA NDALUHERA, kilichopo mtaa wa NDANGARA MULEBA MJINI. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba PHQ/K-AG/BUK/2802/2023, kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba 0786171880.

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI......462......LA 2023**
**VIRINDER KUMAR WATTS...............MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KHUZAIMA SADIKALI MOHAMED.........MDAIWA/WADAIWA**
**WITO KUITWA SHAURINI**
**KHUZAIMA SADIKALI MOHAMED**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

VIRINDER KUMAR WATTS amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala) . Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 31/10/2023 saa 03:00 Asubuhi/mchana mbele ya Mh J.W.SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 24 Mwezi 10/2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI
IDARA YA UHAMIAJI

**MAOMBI YA URAIA**
**HII NI KWA TAARIFA KWAMBA**



**LINDA ACHIENG MATORO**
**S.L.P 14974**
**DAR ES SALAAM.**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mhe. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MKENYA. Nchi atokayo ni KENYA. Shughuli zake ni ...... anwani ya mwajiri..... Yupo hapa nchini tangu mwaka 2003 (miaka 20) Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa kwa maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN. 21 DAR/36290

..............................................................

***Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 82/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU MOHAMED SHABANI MBWANA wa NKUHUNGU**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA DUSUKI MOHAMED SHABANI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 15 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo Tarehe 26 Mwezi 10 Mwaka 2023.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.144 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**FRISMILLER UPENDO MSHANA of Mnadani within Dodoma City**
**AND**
**In the matter of application for letters of administration by**
**ERICK LEONARD PIUS**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner thereof.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of 11, 2023

Dated at Dodoma this 26 day of 10, 2023.

Dated at Dodoma this 26 day of 10 2023
RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No...... of 2023**
**In the matter of the estate of the late**
**KICHELE MWITA KAHINDA**
**of Area D within Dodoma Region.**
**And**
**In the matter of the application for letters of administration by NEEMA KICHELE MWITA**
**GENERAL CITTION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

**ALL PERSON** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner

Objections to the grant should be on or before the 15 day of November, 2023

date at Dodoma this 25 day of October, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 127 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late JOHN MTEMI LWAKAJENDE of Image within Dodoma City**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY**
**SEKUNDA MKANYERERE MTEMI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above- named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of 11,2023

Dated at Dodoma this 25 Day of 10, 2023

25 day of 10 2023
RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOEEN EBRAHIM ESMAIL**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA WISH** yenye usajili namba: **T 110 DJH,** CHASSIA NAMBA: **ZNE100264637** na ENGINE NAMBA: **1Z2373307.**kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/ARU/ARU/5506/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GERALD JONATHAN MSHANA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILLUX** yenye usajili namba T 776 AHY, CHASSIS NAMBA: **RNA50019825** na ENGINE NAMBA **12R3012020.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/ARU/ARU/5305/2023**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE No 111 OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE:**
**ANASTAZIA CHUMA HUGO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY:-**

**1: BATSHEBA DIAMOND SAJAAN**
**2: JOSEPH KAMSOPI MDIMI**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 02 day of 11.2023

DATED at MOROGORO this 23 day of 10.2023

Resident Magistrate
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAKOYE SAFARIS LIMITED**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba**T 348 AFE, CHASSIS** NAMBA: **HZJ750022231** na ENGINE NAMBA : **1HZ013076.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/ARU/ARU/5305/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWAMJA


KIAPO KUTHIBITISHA KUWA HATI (OFFER) YA KIWANJA NA.120 KTALU "A" MNYANJANI IMEPOTEA

MIMI HUBA TWAHA HESHIMA SHEHE wa MAKORORA TANGA, MTU MZIMA MWANAMKE, MUISLAMU, ninathibitisha kwa kiapo na kutamka kama ifuatavyo:-

- KWAMBA, mimi ni mtoto wa marehemu TWAHA HESHIMA SHEHE ambaye alifariki TAREHE 29/5/2010
- KWAMBA, baada ya kufariki kwake niliteuliwa msimamizi wa mirathi yake Na.13/2012 katika Mahakama ya MWANZO ya MWANG'OMBE TANGA.
- KWAMBA, marehemu baba yangu alikua anamiliki kiwanja NA.120 KITALU "A" MNYANJANI katika jiji la TANGA
- KWAMBA, ninatoa kiapo hiki kuthibitisha kuwa hati hiyo (OFFER) hiyo imepotea, na jitihada zangu za kuitafuta imeshindikana kabisa na nmetoa taarifa polisi yenye kumbukumbu, PHQ/TAN/TAN1620/2023
- KWAMBA, ninatoa kiapo kuthibitisha kuwa hati hiyo kweli imepotea na haijawahi kuwekwa kama dhamana au rehani mahali popote kama benki, kwaajili ya kujichukulia mkopo.

NA ninatoa kiapo hiki kuthibitisha na kutamka kuwa yote niliyoyasema katika kiapo hiki ni kweli tupu na kwa mujibu wa sheria za viapo, OATHS ( JUDICIAL PROCEEDINGS) and STATUTORY DECLARATION ACT, CAP.34 R.E.E2019.

## KUPOTEA KWA VYETI



JACOB NYERERE GADIYE anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2206-0063, kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia MEASKRON SECONDARY SCHOOL mwaka 2016 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0150-0528 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia SAME SECONDARY SCHOOL mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: PHQ/MBE/MBE/4224/2023 PHQ/MBE/MBE/4225/2023

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu STANFORD TUMAINI NDALUHEZA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari lenye namba za usajili T 372 BKK yenye majina ya YOSIA KARIJA NDALUHERA. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba PHQ/KAG/BUK/2801/2023, kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au apige simu namba 0786171880.

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-32

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Kundi la nne kuja jamaa wanaitwa 'cold blood killers'. Hawa ni watu wa kuogopwa mno kama ukoma. Ni kama vile hawana roho wala hisia. Ni kama hawakuzaliwa binadamu ila ni wanyama waliojivika ngozi ya binadamu. Wakati mwingine unaweza kusema wana matatizo ya akili. Wao huua taratibu na kwa mateso makubwa mno. Hawa ndiyo wale watu ambao utasikia wamemuua mtu na kuwatenganisha viungo kimoja baada ya kingine. Anaweza kuua kwa leo kukukata kidole, mkono, mguu, kila siku kimoja kimoja hadi mhusika atakapokufa kifo cha mateso. Wapo wanaokwenda mbali zaidi, wanaweza kujirekodi na hata wakati mwingine kupika viungo.

Namba tano ni wauaji kwenye msongo wa mawazo 'stress,' au maumivu ya mapenzi. Wauaji hawa hufikia kuona kila mmoja ni adui yake. Anaweza kuchukua silaha na kwenda hadi kwenye kadamnasi ya watu na kuwafyatulia risasi kwa raha zake. Na mara nyingi watu hawa na wao huishia kujimaliza wao wenyewe watakapobakisha risasi ya mwisho kwenye bastola.

Mauaji ya Tessy yanaingia kwenye aina hizo mbili namba nne na tano, hakuna mtu anayetenganisha kiungo cha mtu kwa kutaka tu kuiba au kuchukua pesa. Ni lazima mauaji alikuwa na hasira kali, ama ni mtu ya aliyedhulumiwa, au wivu mkali ya kimapenzi. Kwa maana hiyo nilimtafuta kwanza mjomba wa marehemu, akanipa majina ya watu ambao niliona nianze nao upelelezi, mmoja wapo ni mume wa marehemu Charton."

"Ukaanza na nani?"

"Yeye huyo huyo Charton. Kile kitendo cha kwenda semina Mwanza, akabaki huko huko badala ya kurudi na wenzake Dodoma, halafu mtu wangu pale Uwanja wa Mwalimu Julius Nyerere akaninyonyea na kunipa video akionekana yupo Dar, na kesho yake akapanda tena ndege kurudi Dodoma na siku aliyotua Dar ndiyo mkewe alipotea, ilinipa shaka na kukaanza kumfuatilia.

Nikagundua hakulala Mwanza, lakini alimlipia mtu na mwanamke wake walale kwa kutumia jina lake, kwa hiyo kuna kitu alitaka kuficha. Alichokuwa akificha ni ushahidi ili ionekane siku mkewe alipotoweka alikuwa Mwanza. Hivyo vyote vipo kwenye ushahidi na nimekusanya vizuri.




**Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ndiye aliyeonekana kwenye televisheni na sauti yake kusikika kwenye redio.**

Kifupi watuhumiwa wetu ni watatu, Charton Antony, mume wa Tessy, Tinga Patauli, na Rukia Hamadi."

Inspekta Frank alipokea vielelezo vyote na kumshukuru sana Eddy Kamal.

"Hapa Eddy sina hata la kumwambia, umeniheshimisha na kesho tutawatangazia umma kuhusu tulio hili ambalo limegusa mioyo ya wananchi na wamekuwa wakisubiri kwa hamu upelelezi wake."

"Sawa ila naomba yule rafiki yangu aliyebebeshwa mzigo wa maiti, Mboneka Fisimaji muachieni huru. Mimi nilitaka akae ndani mpaka wahusika wote wakamatwe kwa sababu iwapo angetoka nje angeweza kuwaambia wenzake, au hata kama asingewaambia, wangejua wale wangeweza kumuua kwa kuwataja."

"Sawa Eddy, nadhani kazi iliyobaki ni kumtoa ndani Charton na mpenzi wake Rukia, Tinga yeye tayari tumeshamkamata."

**************************************

Vipindi vyote vilikatishwa kwenye televisheni na redio zote. Wananchi walishangazwa na hilo. Walishtuka kwa sababu hakujua nini kitaenda kuzungumzwa.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ndiye aliyeonekana kwenye televisheni na sauti yake kusikika kwenye redio.

"Ndugu wananchi mnakumbuka kuwa miezi minane iliyopita maeneo ya Kinondoni Msisiri kulikutwa vipande vya mwili wa binadamu. Na katika uchunguzi ilibainika ni ya mwanamke na jina lake ni Tessy Temu. Viungo vyake vilikuwa vikatwakatwa, kutiwa kwenye viroba na kutelekezwa huko. Baada ya upelelezi na muda mrefu hatimaye tumefanikiwa kukamata watu watatu wanaotuhumiwa kuhusika na mauaji hayo.

Watu hao ni Charton Antony ambaye ni mume wa marehemu. Wa pili ni Tinga Patauli, na wa tatu ni Rukia Hamadi.

Hawa wote tayari wameshakamatwa na wanatarajiwa kufikisha mahakamani hivi karibuni.

Tunapenda kuwaambia wananchi kuwa Jeshi la Polisi limekusanya ushahidi wa kutosha ambao itaupeleka mahakamani na ina uhakika haki itatendeke," akamaliza kamanda huyo.

Hatimaye Jeshi la Polisi sasa lilimaliza kiu ya wananchi ambao kwa muda mrefu lilikuwa linataka liwasake wote waliohusika na kumuua kinyama mwanamke huyo.

Gumzo sasa lilikuwa ni Charton. Yaani mume kumuua kinyama namna ile mkewe. Kamanda aliongea kwa kifupi kwa sababu ya kutotaka kuongea mambo ambayo yangekwenda kuongelewa kama ushahidi mahakamani, lakini kila mtu alifahamu kuwa sababu kuwa itakuwa ni wivu wa kimapenzi.

************************************

"Ulimuua mkeo kwa kushirikiana na Patauli kwa sababu ya kuonyeshwa picha ya hawara yako Rukia si ndiyo?"

Charton hakujibu kitu

"Sasa nikwambie tu kuwa umefanya kitu cha kijinga sana. Hii picha uliyoonyeshwa ni ya zamani sana. Zamani kabla wewe hujawa na Tessy. Alikuwa na uhusiano na kimapenzi na jamaa mmoja anaitwa Barton, kwa sasa anaishi Uingereza. Walipoachana baada ya miaka miwili ndiyo wewe ukamuona na kumchuku akawa mkeo.

Picha hii ilipigwa zamani sana wakati mkeo akiwa amenawiri kwa sababu ya matunzo mazuri kutoka kwa Barton. Walipoachana mkeo aliathirika sana kisaikolojia kiasi cha afya kutetereka, akakonda, hakuwa na siha nzuri na wakati ulipomuona wewe ndiye alikuwa anarejea taratibu kwenye afya yake ya zamani. Wewe ulipoonyeshwa picha ukadhani ni ya sasa kwa sababu hukuwahi kumuona akiwa amenawiri huko nyuma kabla ya kuwa na wewe. Umedanganywa, wivu ukakuingia ukamuua mkeo."

Yalikuwa ni maneno ya Eddy akimnanga Charton. Baada ya kukamatwa, alitaka aletwe ofisini mwake.

Akiwa chini ya ulinzi Charton alipelekwa kwenye ofisi ya Eddy. Kabla ya kupelekwa mahakamani Eddy alijaribu kumuelezea kosa la kiufundi alilolifanya na kusababisha matatizo yote yale.

"Kumbuka wakati unamtongoza Tessy, shoga yake Rukia huyo uliyekamatwa naye alikuwa anadhania kuwa yeye ndiye angechukua hiyo nafasi.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# NYOTA WATATU GULAMALI CUP 2023 KUTUA YANGA SC

**Na Jumbe Ismailly, IGUNGA**

WACHEZAJI watatu kutoka katika mashindano ya Kombe la Mbunge wa Manonga lililopo katika Wilaya ya Igunga, Tabora wanatarajia kwenda kufanya majaribio ya kujiunga na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imeelezwa.

Ahadi hiyo ilitolewa na Rais wa Yanga, Hersi Saidi alipokuwa akizungumza kwa njia ya simu wakati mashindano ya kombe hilo yenye lengo la kuibua vipaji vya vijana yakiendelea.

Hersi alisema uamuzi huo umetokana na vipaji vilivyoonyeshwa na wachezaji wanaocheza michuano hiyo na kuisifu Tabora imetoa nyota mbalimbali wenye vipaji akiwamo Mkurugenzi wa Michezo, Ali Mayai.

Rais huyo alisema Yanga itagharamia safari ya wachezaji hao watakaopitishwa na wakifaulu majaribio, watasajiliwa na vigogo hao wa soka nchini.

"Tumewakosa wengi watu wa Tabora hivyo kwa hatua ya kwanza nitawachukua wachezaji bora watatu kati ya wachezaji wa timu zilizoshiriki mashindano haya kuja kufanya majaribio ndani ya Yanga, baada ya kufuzu nitawasajili kuichezea timu yetu," alisema rais huyo na kuibua shangwe kwa wananchi waliofurika kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Ziba.

Mbunge wa Jimbo hilo, Seif Gulamali ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Yanga alisema anazipongeza timu zote zilizojitokeza kushiriki mashindano hayo ya mwaka huu.

Gulamali alisema kati ya majiko 200 ya gesi waliyokabidhiwa katika ziara ya Rais, Samia Suluhu Hassan, timu zilizoingia nusu fainali na fainali kila timu moja itapatiwa jiko moja.

Akikabidhi kikombe pamoja na zawadi mbalimbali kwa washindi, Mkuu wa Wilaya ya Igunga, Sauda Mtondoo aliwataka wajumbe wa kamati ya mashindano hayo kutofanya upendeleo wakati wa kuchagua wachezaji watakaokwenda kufanya majaribio Yanga.

Mtondoo alisema nyota wengine sita watakaong'ara watakwenda kujiunga na Timu ya Mkoa wa Tabora inayoshiriki Ligi Kuu na wengine watasajiliwa katika kikosi cha timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17.

Mashindano hayo yameshirikisha zaidi ya timu 400 kutoka katika jimbo hilo ambalo lengo lingine ni kuwasaidia kupata ajira.

Young City imefanikiwa kutwaa ubingwa na kupewa zawadi ya Sh. milioni 1.5, ikifuatiwa na Ntobo FC iliyopata Sh. milioni moja na Mwamala ilimaliza katika nafasi ya tatu imejinyakulia Sh. 500,000.



Wachezaji wa Mtibwa Sugar wakifurahia baada ya timu yao kupata bao la tatu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro. Mtibwa Sugar ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# Morogoro yaiota AFCON 2027

**Na Christina Haule, Morogoro**

BAADA ya Tanzania kutangazwa kuwa mwenyeji wa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027), Uongozi wa Halmshauri ya Manispaa ya Morogoro unajipanga kuongeza uchumi kwa kujenga uwanja mkubwa wa mpira ili kukidhi mahitaji ya viwanja vya michezo vitakavyotumika katika fainali hizo.

Akizungumza kwenye kikao cha Baraza la kawaida la madiwani, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Ally Machela alisema tayari wameshatenga kiwanja katika eneo la Kiyegea na sasa wanasubiri wadau watakaosaidiana kupatikana fedha za ujenzi katika bajeti ijayo ili kukuza mapato ya Halmashauri.

Awali Diwani wa Kata ya Mindu, Zuberi Mkalaboko alisema anampongeza Rais, Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika nchini.

Alisema licha ya mikoa iliyotengwa kufanyika michuano hiyo kuwa ni Arusha na Dar es Salaam, ni vizuri Morogoro ambao ni jirani na Dar es Salaam wakajenga uwanja mkubwa na wa kisasa utakaoshawishi baadhi michezo kufanyika hapo.

"Tunaweza kutumia hii fursa, kama tutakuwa na uwanja wetu wenye ubora na viwango vinavyotakiwa, tunaweza kuvishawishi vyombo husika ( Serikali, TFF na CAF), kuhamisha baadhi ya michezo kwenye mkoa wetu, hii itatufanya tuupe thamani kubwa na kutangaza vivutio vyetu," alisema Makalaboko.

Tanzania, Kenya na Uganda zitaanza fainali hizo za AFCON kwa mara ya kwanza baada ya kuwasilisha maombi ya pamoja.

## Aiyee, Edgar wababe Ligi ya Championship

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Mwadui FC, Salim Aiyee anaongoza kwa upachikaji mabao katika Ligi ya Championship ambayo iko kwenye raundi ya saba.

Hata hivyo, Aiyee ambaye kwa sasa anaichezea Mbuni FC, anafungana na wenzake wawili wote wakiwa na mabao matano kila mmoja.

Wachezaji hao ni, Edgar William wa KenGold na Maulid Khalid wa Mbeya City, zote za jijini Mbeya.

Aiyee ambaye alitamba Ligi Kuu msimu wa 2018/19 akiwa na Mwadui FC, akipachika mabao 18 ana 'hat-trick' moja katika ligi hiyo ambayo aliipata wiki iliyopita, timu yake ikiiadhibu Ruvu Shooting magoli 5-0.

Straika Helbert Lukindo wa Biashara United ambaye ana mabao manne anafuatia katika orodha hiyo ya wafungaji wakati Abdulkarim Segeja wa Copco, Damas Makwaya, Kassim Shaibu (Green Warriors), Khalifa Nolo (Stand United), Emmanuel Mpuka (KenGold), Kika Salum (Pan African), na Denis Mushi wa Polisi Tanzania kila mmoja ana mabao mawili.

## Coastal Union yaanza 'nyodo'

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushinda mabao 2-0 dhidi ya Mashujaa FC, ikiwa ni ushindi wake wa kwanza wa Ligi Kuu msimu huu, Coastal Union imesema ndiyo imeanza ligi hiyo na ikizitahadharisha timu zote watakazokutana nazo.

Coastal Union imesema imeanza kupata ushindi baada kusaka na kutambua kilichokuwa kinawatafuna.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Abass El Sabri alisema ushindi huo umepatikana baada ya vikao ya 'usiku na mchana' vilivyohusisha viongozi wa klabu pamoja na benchi la ufundi.

"Ni ushindi wa kujivunia kwa wanachama na mashabiki wote wa Coastal Union kwa sababu haikuja hivi hivi, umetafutwa. Umetafutwa kwa maana baada ya kutoshinda mechi sita, viongozi wanaona haiwezekani, wakamweka kwanza kocha mkuu pembeni, mechi ya sita ambayo tulitoa sare dhidi ya Ihefu hakuwapo na hii pia tuliyoshinda, kwa hiyo nadhani tumeshaanza kujua njia za kupita, sasa tunatangaza rasmi tumeanza ligi," alisema Ofisa huyo.

Mabao ya Coastal Union ambayo sasa iko chini ya Kaimu Kocha Mkuu, Fikirini Elias yalifungwa na Bakari Selemani na Lucas Kikoti.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**BRUYNE ATAKIWA SAUDIA**
MAOFISA wa Ligi Kuu ya Saudia sasa wanamtaka kiungo wa kati wa Manchester City na Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye umri wa miaka 32 kujiunga na ligi hiyo huko Mashariki ya Kati ifikapo mwakani. **(Football Insider)**

**NEVES KUMRITHI TONALI**
KLABU ya Newcastle United inalenga kumnunua kiungo wa kati wa Al-Hilal na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 26, baada ya Sandro Tonali kufungiwa miezi 10 kutokana na kukiuka Sheria ya kamari. **(Sun)**

**GAVI ATAKIWA CHELSEA**
CHELSEA imeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Gavi mwenye umri wa miaka 19, ambaye Barcelona wanaweza kumuuza kwa pauni milioni 87 ili kupunguza matatizo yao ya kifedha. **(Sport kupitia Express)**

**SANCHO ANUKIA SAUDIA**
UHAMISHO wa mkopo kwenda Saudi Arabia ndio njia inayowezekana zaidi ya winga wa Manchester United na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23 kuondoka katika klabu hiyo ingawa Chelsea wanaweza kuwa chaguo huku Borussia Dortmund wakimpuuza. **(Mail)**

**TCHOUAMEN ATAKIWA ARSENAL**
ARSENAL imetanguliza nia ya kumsaini nyota wa Real Madrid na Ufaransa, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 23, msimu ujao huku wakimtafuta kiungo wa kucheza naye pamoja, Declan Rice wa England. **(Football Transfers)**

**ZUBIMENDI KUTUA ARSENAL**
ARSENAL pia wamemtambua Martin Zubimendi wa Real Sociedad kama mchezaji wanayemlenga , ingawa kiungo huyo wa kati wa Hispania mwenye umri wa miaka 24 pia anaivutia Manchester United. **(Football Transfers)**

**INACIO KUTUA LIVERPOOL**
LIVERPOOL imepewa nafasi kubwa ya kumsajili beki wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Goncalo Inacio mwenye umri wa miaka 22 kutoka Sporting Lisbon. **(Bild)**

**ADARABIOYO KITAELEWEKA**
BEKI wa Fulham, Tosin Adarabioyo yuko tayari kuzungumzia mkataba mpya wa muda mrefu baada ya kuona Kocha, Marco Silva akisaini mkataba mpya. Ofa ya Monaco kutaka kumnunua nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 ilikataliwa msimu uliopita, huku Tottenham pia wakivutiwa. **(Standard)**

**DIMARDO RASMI SOKONI**
NEWCASTLE United ndio klabu ya hivi punde zaidi ya Ligi Kuu England kufikiria kumnunua, Federico Dimarco wa Inter Milan, huku mlinzi huyo wa Italia mwenye umri wa miaka 25 akizivutia Chelsea na Manchester United. **(Fichajes)**

**TONALI KUKATWA MSHAHARA**
KLABU ya Newcastle inachunguza uwezekano wa kupunguza mshahara wa Sandro Tonali baada ya kiungo huyo wa kati wa Italia mwenye umri wa miaka 23, kufungiwa miezi 10 kwa kucheza kamari. **(Telegraph)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# OSIMHEN: NITACHEZA MAREKANI SIO SAUDIA

●●●Akataa ofa nono ya Al Hilal, Liverpool, Spurs zatajwa...

**NAPLES, Italia**

MSHAMBULIAJI wa Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen amesema afadhali kucheza Ligi Kuu ya Soka Marekani (MLS), kuliko kuelekeka Ligi ya Saudia.

Osimhen mwenye umri wa miaka 24, alikuwa na ofa nono kutoka kwa klabu ya Saudia ya Al Hilal msimu huu wa joto ambayo iliripotiwa kukataliwa na Napoli.

"Nina furaha nikiwa Napoli," alisema Osimhen katika mahojiano yake na Twitch.

"Watu hawajui jinsi ilivyo ngumu kucheza Serie A. Kwa mtazamo wa kimbinu na kimwili, ni moja ya ligi ngumu zaidi kucheza."

Alipoulizwa kama angependelea kucheza MLS au Saudi Pro League ikiwa atapewa ofa nzuri, Osimhen alisema: "Nitachagua kucheza Marekani."

Hata hivyo, Osimhen aliisifu Ligi ya Saudi Pro League.

Tangu kuwasili kwa Cristiano Ronaldo katika klabu ya Al Nassr Januari, mwaka huu, Ligi ya Saudia imevutia baadhi ya wachezaji wenye majina makubwa wakiwamo mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or 2022, Karim Benzema na mshambuliaji wa Brazil, Neymar Jr.

Msimu uliopita klabu za Saudi zilitumia karibu dola bilioni moja kupata wachezaji 94 kutoka katika Ligi Kuu mbalimbali za Ulaya.

"Wanajaribu kukuza ligi yao, ambayo ni nzuri," aliongeza Osimhen ambaye sasa anatajwa kuwindwa na Tottenham Spurs, Liverpool na Chelsea.

"Mmoja Ronaldo bora wa wakati wote amekwenda huko. Kwa sababu ya ushawishi wake Ronaldo amevutia wachezaji wengi wenye vipaji pia kwenda huko. Kwa hiyo kwangu ni nzuri sana, wanajaribu kujenga ligi yao kuwa bora zaidi. Kwangu mimi wanafanya jambo la kuvutia."

Osimhen bado hajafanya uamuzi kuhusu mustakabali wake. Licha ya miezi kadhaa ya mazungumzo ya kurefusha mkataba, mchezaji huyo bado hajaweka wazi juu ya mkataba mpya na makubaliano yake ya sasa yanamalizika ifikapo Juni, 2025.

Napoli bado wana matumaini Osimhen atasaini mkataba mpya licha ya klabu hiyo kudai mchezaji huyo ana "mawazo ya pili" kuhusu kuendelea kuitumikia klabu hiyo baada ya mwaka 2025.

Osimhen, ambaye alijiunga na Napoli msimu wa joto wa 2020 akitokea Lille, alifunga mabao 31 msimu uliopita na kuwasaidia kushinda taji la Serie A kwa mara ya kwanza baada ya miaka 33.

# ONANA AFUNGUKA GARNACHO HAJAKOSEA

**MANCHESTER, England**

ANDRE Onana amemtetea mchezaji mwenzake wa Manchester United, Alejandro Garnacho baada ya Chama cha Soka cha England (FA), kuanzisha uchunguzi kuhusu chapisho la mtandao wa kijamii lililotolewa na raia huyo wa Argentina akiwa na sokwe wawili juu ya picha ya kipa huyo wa Cameroon.

Garnacho aliandika chapisho hilo kwenye X, ambayo zamani ilikuwa Twitter, baada ya Onana kuokoa penalti ya dakika za lala salama na kuipa United ushindi wa bao 1-0 dhidi ya FC Copenhagen kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mapema wiki hii.

Ilifutwa muda mfupi baadaye baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 kufahamishwa na klabu kuhusu uwezekano wa kuhusishwa na ubaguzi wa rangi.

FA inachunguza tukio hilo na imemtaka Garnacho kwa uchunguzi wake.

Alejandro Garnacho ameichezea Manchester United mechi 11 hadi sasa msimu huu.

Siku ya Alhamisi, Onana alimtetea Garnacho katika chapisho lake kwenye mtandao wa kijamii.

"Watu hawawezi kuchagua kile ninachopaswa kuchukizwa nacho," alisema Onana kwenye Instagram.

"Ninajua hasa Garnacho alichokuwa anamaanisha: nguvu na nguvu. Jambo hili halipaswi kwenda mbali zaidi."

Garnacho anaweza kufungiwa iwapo atashtakiwa na FA kwa kukiuka sheria zake.

Mnamo 2019, kiungo wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva alifungiwa mechi moja na kutozwa faini ya pauni 50,000 na FA baada ya kumlinganisha Benjamin Mendy na katuni nyeusi, licha ya tume kukubali hakukusudia kuwa mbaguzi wa rangi.

Mwaka 2021, mshambuliaji wa United, Edinson Cavani alipewa adhabu ya kutocheza mechi tatu na kutozwa faini ya pauni 100,000 kwa chapisho la mtandao wa kijamii ambalo lilikuwa na neno la Kihispania ambalo lingeweza kutafsiriwa kama ubaguzi wa rangi nchini England.




# Klopp akunwa na Núñez

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema amefurahishwa na umaliziaji wa Darwin Núñez (24), baada ya fowadi huyo kukosa bao la wazi huku klabu hiyo ya Merseyside ikiendeleza rekodi nzuri katika Ligi ya Europa msimu huu kwa ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Toulouse hapo juzi.

Mchezaji huyo ambaye alihamia Liverpool akitokea Benfica ya Ureno kwa mkataba wa awali wa euro milioni 75 Juni, mwaka jana alikosa nafasi ya kufunga bao lake la pili usiku huo, lakini ilifanya vyema kwenye Uwanja wa Anfield.

Baada ya kufunga kipindi cha kwanza, Núñez aliisaidia Liverpool kusonga mbele kwa pointi tano kileleni katika Kundi E.

Diogo Jota, Wataru Endo, Ryan Gravenberch na Mohamed Salah wote walifunga kwenye mchezo huo.

"Alicheza vizuri sana. Kusema kweli, katika wakati huu, sikujali hata kidogo kugonga nguzo wakati huo kwa sababu kila kitu hapo awali kilikuwa cha kushawishi, kilikuwa wazi kabisa," alisema Klopp.

Kocha huyo alisema kuna mengi zaidi yanakuja kutoka kwa kiungo wa kati Gravenberch mwenye umri wa miaka 21, ambaye alijipenyeza kwenye kona muda mfupi baada ya Nunez kukosa.

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Gravenberch kuanza mfululizo baada ya miezi 18, baada ya kujiunga kutoka kwa mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich.

"Ninampenda sana kama mvulana na kama mchezaji, na inapendeza sana kuona ni kiasi gani anaanza kujiamini tena. Ni wazi ni muhimu sana kwa kila mchezaji lakini kwa mchezaji mchanga ina maana sana," Klopp alieleza kuhusu Gravenberch.

# Tonali afungiwa miezi 10, sasa kuikosa Euro 2024

**ROME, Italia**

KIUNGO wa kati wa Newcastle United, Sandro Tonali amefungiwa kujihusisha na soka kwa muda wa miezi 10 kutokana na kukiuka sheria za kamari katika mechi nchini Italia, Mkuu wa Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), alisema juzi.

Tonali mwenye umri wa miaka 23, ambaye alijiunga na Newcastle akitokea AC Milan kwa mkataba euro milioni 70 na nyongeza mwaka huu, lazima pia ahudhurie vikao vya matibabu ya uraibu wa kamari kwa kipindi cha miezi nane kama sehemu ya makubaliano na FIGC.

Makubaliano ya mazungumzo, ambayo yanatarajiwa kutumika duniani kote, yalithibitishwa na Rais wa FIGC, Gabriele Gravina.

Kufungiwa kwa Tonali maana yake atakosa kipindi kilichosalia cha msimu huu na michuano ya Euro 2024 msimu ujao wa joto.



Tonali ndiye mchezaji mashuhuri zaidi aliyekumbwa na kashfa ya kamari ambayo inatikisa soka la Italia.

Kanuni za FIFA na FIGC zilimaanisha Tonali angeweza kukabiliwa na kusimamishwa kwa miaka mitatu, lakini ushirikiano wake na mamlaka zinazoongoza uchunguzi, FIGC na ofisi ya mwendesha mashtaka wa Italia ulisababisha kupunguzwa kwa adhabu yake.

Yeye ni mmoja wa wanasoka watatu wa Italia ambao shughuli zao za kamari zimechunguzwa na mamlaka.

Tonali na mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Italia, Nicolò Zaniolo walitolewa katika kambi ya Italia Oktoba 12, mwaka huu baada ya kuarifiwa na polisi kuhusika mchezo wa kamari.

Wachezaji wote wawili walishiriki Ligi Kuu ya England ya wikendi iliyopita, huku Tonali akitokea benchi kwa Newcastle, na Zaniolo akiichezea Aston Villa kwa dakika 76.

Wakala wa Tonali, Giuseppe Riso, alisema wiki iliyopita mchezaji huyo "anapigana na uraibu wa kucheza kamari" na "ameshitushwa na huzuni" kutokana na hali yake.

ESPN iliripoti wiki iliyopita kiungo wa Juventus, Nicolo Fagioli alifungiwa miezi saba na miezi mitano ya ziada kwa kukiuka sheria za kamari na pia alipigwa faini ya euro 12,500.

HABARI MICHEZO

# SHIME AAHIDI MAKUBWA TWIGA IKIENDA BOTSWANA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime amewapongeza wachezaji wake kwa kupata ushindi na anaimani pia itafanya vyema katika mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki dhidi ya wapinzani wao Botswana.

Twiga Stars ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Botswana na timu hizo zitarudiana Oktoba 31, mwaka huu jijini Gaborone.

Akizungumza mara baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mchezo huo, Shime alisema Botswana walionyesha upinzani mkubwa kwa sababu wanajuana na juzi ilikuwa ni mara ya nne kwa timu hizo kukutana.

Shime walijua aina ya mchezo wanaocheza Botswana hivyo walijipanga mapema namna ya kuwakabili na anawapongeza wachezaji wake kwa kufuata maelekezo ambayo yalisaidia kupata ushindi.

"Mechi ilianza kwa mshutuko na tulifanikiwa kupata bao la mapema ambalo hatukutarajia, kipindi cha kwanza tulikamata mpira na Botswana walicheza mpira wa chini.

Changamoto yetu safu ya kiungo tumekua tukipiga pasi nyingi sana, kando na nyuma zilichelewa kuwafikia washambuliaji na eneo la wapinzani. Kipindi cha kwanza hatukutengeneza pasi hatarishi kwa wapinzani wetu, kipindi cha pili tuliongeza nguvu ya kufanya mashambulizi, Botswana walikuja kivingine," alisema Shime.

Aliongeza mabadiliko aliyofanya yalisaidia kupata bao la pili dakika za mwishoni na yeye siku zote ni muumini wa kushinda hata katika mchezo wa marudiano utakaochezwa ugenini.

"Mchezo wa mpira unategemea kucheza vizuri na kushinda bao 1-0, unaweza kumwondoa mpinzani wako, sio lazima kufunga mabao 5-0 ndio umtoe, unapokuwa na timu nzuri unaweza kutafuta ushindi nyumbani na kutafuta bao ugenini, ninafuraha kubwa kwa sababu tumeshinda nyumbani na hatujaruhusu bao," alisema Shime.

Kocha huyo aliongeza wanakwenda ugenini kutafuta bao kwa sababu wana safu ya ushambuliaji na ulinzi imara huku akisema baadhi ya wachezaji walichelewa kujiunga kambini sasa watapata nafasi nzuri ya kufanya mazoezi pamoja na wenzao kabla ya kuanza safari.



Mshambuliaji wa Twiga Stars, Opa Clement (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Botswana katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. Twiga Stars ilishinda mabao 2-0. **PICHA : TFF**

# TCAA Marathon kufanyika kesho

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila anatarajia kuongoza mbio za hisani zilizoandaliwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) zitakazofanyika kesho katika viwanja vya Mlimani City, Dar es Salaam.

Zaidi ya wanariadha 400 wanatarajiwa kushiriki mbio hizo ikiwa ni mwendelezo wa matukio ya kusherehekea miaka 20 ya taasisi hiyo ambayo imepiga hatua katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Mwenyekiti wa maadhimisho hayo, Mellania Kasese amesema lengo lao ni kutunisha mfuko wa upandaji miti katika maeneo yenye ukame.

"Mbio hizo zitakuwa za kilomita tano na 10, maandalizi yameshakamilika na vifaa vyote vimeshafika mpaka sasa tunavyoongea tiketi zote 400 ambazo zilitengwa kuuza kwa ajili ya washiriki zimeshaisha siku tatu nyuma,"alisema Kasese.

Naye Katibu wa Chama Cha Riadhaa Mkoa wa Dar es salaam (DAAA), Samweli Mwela ambao ni wasimamizi wa mbio hizo amesema chama hicho kinashirikiana vyema na TCAA katika maandalizi ya mbio hizo na amewataka wadau kujitokeza.

"Tumejiridhisha na tumehakikisha njia zitakazotumika kwanza zimepimwa na salama, tunasubiri Jumapili ifike kwa ajili yakuhitimisha tukio lenyewe," alisema Mwela.

Aidha alitoa wito kwa wadau wengine wanaoandaa mbio za hisani kushirikiana na chama hicho ili kuepukana na chagamoto mbalimbali zinazojitokeza kwa kukiuka kanuni na taratibu.

"Ni hatari ukipata jambo utakuwa hauna pakupeleka, tunashukuru TCAA imetushirikisha, wamefanya vizuri na wanajua nini chakufanya," Mwela alisema.

## Wadau wa Kubeti waomba punguzo

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa Michezo ya kubahatisha na makampuni ya kubashiri michezo mbalimbali wameiomba serikali kupitia upya sheria zilizopo sasa za uendeshwaji wa michezo hiyo ili kuwapunguzia mlundikano wa kodi wanazotozwa.

Wakizungumza kwenye kongamano lilioandaliwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) mbele ya Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Chande walisema sheria za sasa zinawabana zaidi waendeshaji wa michezo hiyo.

Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Kampuni ya Sportpesa, Tarimba Abass alisema kwa sheria inatoa nafasi kwa serikali kunufaika kwanza bila kujali mwekezaji amekiingiza kiasi gani.

"Michezo ya kubahatisha inapaswa kuendeshwa na taasisi mama pekee ambayo ni GBT, lakini taratibu za sasa zipo taasisi nyingine za serikali zina mamlaka ya kusimamia, lakini pia tunaomba serikali iangalie namna ya kupunguza mzigo wa kodi kwa wawekezaji kwa maana ya makampuni haya yanayoendesha michezo hii," alisema Tarimba.

Naye Mkurugenzi wa GBT, James Mbalwe alisema kwa sasa sekta ya michezo ya kubahatisha na utabiri wa michezo inaliingizia fedha nyingi serikali kupitia kodi wanayokatwa.

"Kwa sasa tumefikia kulipa au kuchangia kiasi cha Sh. bilioni 170 kwenye pato la taifa zitokanazo na kodi, hii inaonyesha namna sekta hii inavyokuwa kwa kasi," alisema Mbalwe.

Akitoa neno la serikali kwenye kongamano hilo, Naibu Waziri wa Fedha, Chande aliiagiza GBT na bodi yake kuangalia namna wanavyoweza kupunguza 'mzigo' wa kodi kwa makampuni hayo ili kila upande unufaike na uwekezaji huo.

"Lakini pamoja na hayo naomba sana wawekezaji katika sekta hii kufuata sheria na taratibu zilizowekwa katika kusimamia michezo hii, tunaomba muwe mabalozi wazuri kwa kuhakikisha sheria hazivunjwi na kila mmoja anafuata taratibu, makampuni yasiyokuwa na leseni ya uendeshaji myataje ili yachukuliwe hatua" alisema Chande.

Alisema serikali haitamwonea mtu au kampuni inayofuata taratibu katika uwekezani wake na imejipanga kutoa ushirikiano unaohitajika.

Kongamano hilo lilifanyika katika kushereheke kumbukizi ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa GBT hapa Tanzania.

Michezo
Jumamosi Oktoba 28, 2023
Nipashe




UK. 21

## Osimhen: Nitacheza Marekani



Jezi mpya zitakazovaliwa katika mechi za nyumbani za Timu za Soka za Taifa ambazo zilizinduliwa rasmi jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: TFF**

# Yanga yaendeleza dozi

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Mabao mawili ya Maxi yawaimarisha katika msimamo na...

MABAO mawili yaliyofungwa kipindi cha kwanza na kiungo mshambuliaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Maxi Nzengeli yaliwapa ushindi wa magoli 2-0 mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga dhidi ya Singida Fountain Gate katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Maxi alifunga bao la kwa kichwa dakika ya 30 likiwa ni goli la kwanza pia kwa Yanga kufungwa kwa kichwa tangu kuanza kwa msimu huu baada ya mechi sita, kabla ya hapo mabao 18 yaliyofungwa hadi raundi hiyo yalifungwa kwa miguu na wachezaji.

**Mchezaji huyo pia anafikisha mabao sita akiwa juu ya kilele cha orodha ya wafungaji sawa kiungo mshambuliaji wa vinara hayo, Stephane Aziz Ki.**

Mabao matatu amefunga kwa mguu wa kulia, mawili kushoto na moja la kichwa, matano akiyafunga ndani ya eneo la hatari na kwa mara ya kwanza jana alifunga bao la pili nje ya eneo boksi.

Ushindi huo umewafanya mabingwa hao kufikisha pointi 18 na kuendelea kuongoza katika msimamo huku ikiwa na mabao 20 kibindoni.

Yanga ilianza mechi kwa kuliandama lango la Singida Fountain Gate na dakika ya saba tu krosi ya Pacome Zouzoua ilileta kizaazaa kwenye langoni la wageni hao huku kipa, Benjamin Haule akiwa ametoka lakini wachezaji, Mudathir Yahaya na Hafiz Konkoni walishindwa kuuweka mpira wavuni.

Singida FG ilijibu shambulio hilo dakika ya 13, kupitia kwa Kelvin Kijili alipoambaa na mpira kwenye wingi ya kushoto, lakini alipiga krosi fyongo huku wenzake Habib Kyombo na Marouf Tchakei wakiwa peke yao wanausubiri wauweke wavuni.

Pacome kwa mara nyingine tena dakika ya 27, alifanya kazi ya ziada alipowalamba chenga mabeki wa Singida FG na kumwekea Konkoni ndani ya eneo la hatari, lakini shuti lake liliishia katika mikononi ya Haule na ilionekana kama alimlenga.

Hatimaye, dakika ya 30 baada ya jitihada nyingi, Yanga iliandika bao la kwanza lilowekwa wavuni na Maxi Nzengeli aliyemalizia kwa kichwa mpira wa krosi ya Yao Kouassi kutoka wingi ya kulia.

Dakika nane baadaye, Maxi tena alipata mpira umbali ya mita 40 hivi kutoka katika lango la Singida FG, akaanza kuwalamba chenga baadhi ya wachezaji na kabla hajaingia ndani ya eneo la hatari na kuachia kombora kali lililokwenda kushoto kwa Haule na kumwacha asiwe na la kufanya.

Muda huo huo, Haule aliumia na nafasi yake ikachukuliwa kipa namba tatu wa timu hiyo, Ibrahim Rashid ambaye alimaliza mechi hiyo bila kufungwa.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko ya wachezaji kwa nyakati tofauti, Yanga ikiwatoa Mudathir, Pacome, Joyce Lomalisa, na Aziz Ki na kuwaingiza Mahlatse Makudubela 'Skudu', Kennedy Musonda, Nickson Kibabage, Clement Mzize na Salum Aboubakar 'Sure Boy' huku Singida FG ikiwatoa Bruno Gomes, Aziz Andambwile na nafasi zao kuchukuliwa na Meddie Kagere na Mourice Chukwu.

Pia Singida FG ilifanya mabadiliko ya kuwaingiza Denis Kaseke na Kasengu Kazadi.

Mabadiliko hayo kwa kiasi kikubwa yaliwasaidia Singida FG hasa Chukwu ambaye aliituliza timu kwenye kiungo katikati ya uwanja na kuifanya kuhimili dakika 45 za kipindi cha pili bila kufungwa bao lingine.

Hata hivyo ni Singida FG ndiyo iliyokuwa inakoswakoswa na wachezaji wake walionekana kuridhika na matokeo yaliyokuwapo kwa muda mrefu wakiitumia kuzuia zaidi badala ya kwenda mbele kutafuta walau bao la kufutia machozi.

## Simba ya moto kuwavaa Ihefu

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuondolewa katika mashindano ya kimataifa ya Africa Football League (AFL), Simba inatarajia kuwakaribisha Ihefu katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Simba ambayo haijapoteza mechi hata moja msimu huu, itashuka dimbani leo ikiwa na 'moto' ambao iliounyesha katika michuano ya AFL, kwa kuwalazimisha sare mara mbili mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira (Robertinho), amesema ataingia katika mechi hiyo kuendeleza pale alipoachia na kubwa ni kuondoka na pointi tatu ili kurejea kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Robertinho alisema amepata nafasi ya kufanyia kazi changamoto alizozibaini katika mashindano ya AFL na sasa kikosi chake kipo tayari kusaka ushindi na kujiimarisha kileleni.

Alisema siku chache zilizopita wasaidizi wake walifanikiwa kuwafuatilia Ihefu FC ilipocheza dhidi ya Coastal Union na kufahamu wanavyocheza, ubora na madhaifu yao.

"Kila mechi tunahitaji kuwaheshimu wapinzani wetu bila kujali tunacheza na timu inashika nafasi ya ngapi, malengo yetu ni kucheza vizuri na kupata alama tatu ambazo zitaturejesha kwenye nafasi yetu ya kileleni na mwisho wa msimu kutwaa mataji ya ubingwa," alisema Robertinho

Aliongeza anaweza kufanya mabadiliko kidogo katika kikosi chake kwa kuwapa nafasi baadhi ya wachezaji ambao hawajaonekana mara nyingi katika mechi kwa sababu anaendelea kuimarisha kikosi chake cha kwanza.

"Napanga kikosi kulingana na timu ambazo tunaenda kukutana nazo na jinsi ya misingi ya wachezaji niliokuwa nao, hivi leo (jana), nikimweka benchi Baleke (Jean) wataniuliza kwanini nampa nafasi Phiri (Moses) na kumweka benchi?" alihoji Robertinho.

Moses Basena, Kocha Mkuu wa Ihefu alisema timu yake imejiandaa vizuri kuikabili na Simba, wanatambua wanakutana na timu nzuri ambayo imetoka kwenye mashindano ya AFL.

"Kwa wiki mbili tangu nimekabidhiwa kukinoa kikosi cha Ihefu, kuna jambo nimelifanya na ninaimani tutaonyesha upinzani mkubwa mbele ya Simba," alisema Basena.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >